# MATUMIZI YA LUGHA KATIKA MUZIKI WA KIZAZI KIPYA: MIFANO KUTOKA KATIKA NYIMBO ZA MAPENZI ZA WASANII INSPEKTA HAROUN NA MWANAFALSAFA

Na

Adam Hussein Jumbe

Tasnifu Iliyotolewa kwa Ajili ya Mahitaji ya Shahada ya Uzamili ya Sayansi Jamii katika Fasihi ya Kiswahili

Chuo Kikuu cha Dodoma

Oktoba, 2015

## ITHIBATI YA MSIMAMIZI

Aliyetia sahihi hapo chini anathibitisha kuwa amesoma kazi hii na hapa anapendekeza kuwa Chuo Kikuu cha Dodoma kikubali kupokea tasinifu hii: ***Matumizi ya Lugha Katika Muziki wa Kizazi Kipya, Mifano Kutoka Katika Nyimbo za Mapenzi za Inspekta Haroun na Mwanafalsafa*** katika kukamilisha masharti ya Shahada ya Umahiri katika Fasihi ya Kiswahili ya Chuo Kikuu cha Dodoma.

________________________

Dkt. Athumani S. Ponera

(Msimamizi)

Tarehe: ______________________

## IKIRARI NA HAKIMILIKI

Mimi, **Adam H Jumbe**, nathibitisha kuwa tasnifu hii ni kazi yangu halisi na haijawahi kuwasilishwa na haitawasilishwa katika chuo kikuu kingine kwa ajili ya kutunukiwa Shahada kama hii au nyingine yoyote.

Sahihi ………………………

Hairuhusiwi kuzalisha, kutafsiri, kunakiri, kupiga chapa, kuiga wala kusambaza sehemu yeyote ya tasnifu hii kwa namna yeyote ile bila ya ridhaa ya maandishi kutoka kwa mwandishi au Chuo Kikuu cha Dodoma.

## SHUKRANI

Kama ilivyo kawaida, tasnifu hubeba jina la mtu mmoja, lakini ni matokeo ya mchanganyiko wa mawazo ya watu mbalimbali. Si kazi rahisi kuandika kwa undani mchango wa kila mtu aliyesaidia katika kufanikisha na kukamilisha kazi hii. Lakini wafuatao wanastahili shukrani zangu za kipekee. Kwanza kabisa ningependa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuwa nami na kunipa afya njema katika kipindi chote cha masomo yangu. Pia kwa kuniwezesha kuwa na nguvu na welewa wa kufanya utafiti huu.

Pili, ningependa kutoa shukurani zangu za dhati kabisa kwa msimamizi wangu wa tasnifu hii, Dkt. Athumani Salumu Ponera ambaye hakusita kunishauri katika hatua zote za uandishi wa kazi hii mpaka nilipoikamilisha ikiwa katika sura ya kazi bora na yenye mlengo wa kitaaluma tena mmahiri wa Fasihi ya Kiswahili. Asante sana Dkt. Ponera.

Tatu, napenda kuishukuru familia yangu, wazazi wangu, Bwana Hussein Hassani Jumbe na Bibi Zena Ally Kamtande; pamoja na mke wangu, Aziza Goha Athumani; na watoto wangu, Yusrat Adam Jumbe na Nilham Adam Jumbe. Ninawashukuru kwa uvumilivu wenu kwa kipindi chote ambacho sikuwa nanyi. Pia, shukrani zangu ziende kwa ndugu zangu wote katika familia ya Mzee Hussein H Jumbe ambao ni wadogo zangu, Ismail H. Jumbe, Salim H. Jumbe, Rehema H. Jumbe, Mariamu H. Jumbe, Kashinde H. Jumbe, Mwangaza H. Jumbe, Khadija H. Jumbe, Khairuni H. Jumbe na Zawadi H. Jumbe ambao walinisaidia kwa hali na mali katika kipindi chote cha masomo yangu. Mungu awabariki nyote. Naamini bila ya kujitoa kwenu leo hii mimi nisingefika hapa nilipo kitaaluma kwani nyie ni chachu ya maendeleo na mafanikio yangu

## TABARUKU

Naitabaruku kazi hii kwa baba yangu Bwana Hussein Hassani Jumbe na mama yangu Bi. Kulwa Abdallah Mwinyimkuu, kwa kunileta ulimwenguni na kunionesha njia sahihi ya namna ya kuishi na watu, kunilea, kuniongoza na kunisadia katika kutafuta elimu na taaaluma na kuwa nami katika kipindi chote cha masomo, ambapo upendo na maombi yao ndiyo yaliyokuwa nguzo na ngao iliyonisaidia katika mafanikio yangu.

# IKISIRI

Utafiti huu ulichunguza ‘Matumizi ya Lugha Katika Muziki wa Kizazi Kipya: Mifano Kutoka Katika Nyimbo za Mapenzi za Wasanii Inspekta Haroun na Mwanafalsa’. Utafiti ulilenga kubainisha lugha inayotumika katika kusawiri vionjo vya mapenzi, katika nyimbo za wasanii teule wa muziki wa kizazi kipya; kuchunguza sababu zilizowafanya wasanii teule kutumia lugha hiyo katika kusawiri vionjo vya kimapenzi katika nyimbo zao; pamoja na kuchunguza athari ambazo hadhira hupata kutokana na matumizi ya nyimbo zinazobeba dhana ya mapenzi katika jamii. Mbinu ya ufafanuzi ndiyo ilitumika katika utafifiti huu wa kitaamuli huku nadharia ya Umuundo ndiyo iliyotumika katika uchambuzi wa data. Wakati mbinu za ukusanyaji data zilizotumika katika kuukamilisha utafiti huu ni udurusu wa kimaktaba, ushuhudiaji, usaili wa watafitiwa pamoja na mjadala wa vikundi.

Matokeo ya utafiti huu yamebaini kuwa matumizi ya lugha katika muziki wa kizazi kipya, hususani katika tungo za mapenzi, hutumiwa na wasanii kutokana na sababu mbalimbali kama vile soko la muziki, mapenzi ya wasanii katika tungo hizo na hata kuonesha hisia zao kwa wapendwa wao.Tija zipatikanazo kutokana na utafiti huu ni kuburudisha jamii, kuongeza msamiati wa lugha, kudumisha mahusiano katika jamii. Pia, kuna athari zilizooneshwa kutokan na matumizi ya nyimbo zenye vionjo kama vile kujiingiza katika mahusiano katika umri mdogo, mmomonyoko wa maadili katika jamii na kudumaza kwa ubunifu. Mchango mpya ulioibuliwa na utafiti huu ni kuwepo/kuibuliwa kwa misimu mbalimbali ambayo inazungumzia mapenzi au huonesha vionjo vya mapenzi katika jamii. Vilevile, kwa kupitia utafiti huu nyimbo teule za mapenzi pamoja na taarifa za wasanii hawa wateule zitaweza kuhifadhiwa kwa ajili ya matumizi ya baadaye na watafiti wengine pindi zitakapohitajika.

**YALIYOMO**

ITHIBATI YA MSIMAMIZI ........................................................................ i
IKIRARI NA HAKIMILIKI........................................................................ ii
SHUKRANI........................................................................................ iii
TABARUKU ....................................................................................... iii
IKISIRI ..............................................................................................v
YALIYOMO........................................................................................ vi
ORODHA YA VIFUPISHO........................................................................ ix

**SURA YA KWANZA** ...............................................................................1
UTANGULIZI ..........................................................................................1
1.1 Usuli wa Tatizo la Utafiti........................................................................1
1.2 Tamko la Tatizo la Utafiti........................................................................5
1.3 Malengo ya Utafiti .................................................................................6
1.3.1 Lengo Jumla.........................................................................................6
1.3.2 Malengo Mahsusi...................................................................................6
1.4 Maswali ya Utafiti ..................................................................................7
1.5 Manufaa ya Utafiti .................................................................................7
1.6 Taarifa Fupi za Wasanii Teule.................................................................8
1.6.1 Taarifa Fupi ya Inpekta Haroun.............................................................8
1.6.2 Taarifa Fupi ya Mwanafalsafa ..............................................................8
1.7 Nadharia Iliyotumika Katika Utafiti .........................................................9
1.7.1 Misingi ya Nadharia ya Umuundo...........................................................9
1.8 Muhtasari wa sura ya kwanza...............................................................13

**SURA YA PILI** :**MAPITIO YA MAANDIKO**...................................................14
2.1 Utangulizi..............................................................................................14
2.1 Maandiko Kuhusu Chimbuko na Maendeleo ya Muziki wa Kizazi Kipya .....14
2.2 Maandiko Kuhusu Matumizi ya Lugha na Muziki wa Kizazi Kipya ..................18
2.3 Mapengo Yanayopaswa Kuzibwa ............................................................25

**SURA YA TATU** : **USANIFU NA MBINU ZA UTAFITI** ..........................................26
3.1Utangulizi...............................................................................................26

3.2 Mpango wa Utafiti ........................................................................................26
3.3 Eneo la Utafiti ...............................................................................................26
3.4 Walengwa wa Utafiti .....................................................................................27
3.4.1 Wango Tafitiwa ............................................................................................27
3.4.2 Sampuli ya Watafitiwa..................................................................................27
3.5 Ukusanyaji wa Data .......................................................................................28
3.5.1 Njia na Zana za Ukusanyaji wa Data ...........................................................29
3.5.1.1Udurusu wa Kimaktaba .................................................................................29
3.5.1.2 Ushuhudiaji, Mjadala wa Vikundi na Usaili................................................29
3.5.2 Mchakato wa Ukusanyaji wa Data na Udhibiti Wake ..................................30
3.6 Uchanganuzi wa Data .....................................................................................31
3.7 Uhalali na Uthabiti wa Matokeo ya Utafiti.....................................................31
3.8 Changamoto za Utafiti na Utatuzi Wake ........................................................32
3.9 Mipaka ya Utafiti ............................................................................................32

**SURA YA NNE: MJADALA WA MATOKEO YA UTAFITI** ..........................33
4.1 Utangulizi........................................................................................................33
4.2 Matumizi Ya Lugha Zenye Vionjo Vya Mapenzi Katika Muziki Wa Kizazi Kipya...........................................................................................................33
4.2.1 Muhtasari wa Nyimbo Teule za Inspekta Haroun ..........................................33
4.2.1.1Wimbo wa “Mtoto wa Geti Kali” ..................................................................34
4.2.1.2 Wimbo wa “Asali wa Moyo”.........................................................................37
4.2.1.3 Wimbo wa “Bint Kisura”...............................................................................39
4.2.1.4 Wimbo wa “Asali wa Moyo (remix)”...........................................................42
4.2.2 Muhtasari wa Nyimbo Teule za Mwanafalsafa ..............................................45
4.2.2.1 Wimbo wa “Alikufa kwa Ngoma”.................................................................45
4.2.2.2 Wimbo wa “Wanazimika” .............................................................................48
4.2.2.3 Wimbo wa “Hawajui”....................................................................................50
4.2.2.4 Wimbo wa “Unanitega”.................................................................................53
4.2.3 Vionjo Vya Kimapenzi Katika Nyimbo za Wasanii Teule..............................56
4.2.3.1 Vionjo vya Kimapenzi Katika Nyimbo za Inspekta Haroun .........................56
4.2.3.1(a) Vionjo vya Kimapenzi Katika Wimbo wa Asali wa Moyo.......................56
4.2.3.1(b) Vionjo vya Kimapenzi Katika Wimbo wa “Bint Kisura” .........................57
4.2.3.1(c) Vionjo vya Kimapenzi Katika Wimbo wa “Mtoto wa Geti Kali”.............58

4.2.3.1(d) Vionjo vya Kimapenzi Katika “Wimbo wa Asali wa Moyo (remix)” .......59
4.2.3.2 Vionjo vya Kimapenzi Katika Nyimbo za Mwanafalsafa .............................60
4.2.3.2(a) Vionjo vya Kimapenzi Katika Wimbo wa “Alikufa kwa Ngoma” ............60
4.2.3.2(b) Vionjo vya Kimapenzi Katika Wimbo wa “Wanazimika” ........................61
4.2.3.2(a) Vionjo vya Kimapenzi Katika Wimbo wa “Hawajui” ..............................61
4.2.3.2(a) Vionjo vya Kimapenzi Katika Wimbo wa “Unaitega” .............................62
4.3 Sababu Za Matumizi Ya Vionjo vya Kimapenzi Katika Nyimbo za Wasanii Teule ...........................................................................................................63
4.3.1 Kufikisha Ujumbe ...........................................................................................63
4.3.2 Kunasa/Kuvutia Soko la Biashara ...................................................................63
4.3.3 Athari ya Fasihi pendwa Katika Jamii ............................................................64
4.3.4 Hulka za Binadamu .........................................................................................64
4.4.5 Ithibati ya Uhuru wa Kisanaa .........................................................................65
4.4 Athari Za Vionjo Vya Kimapenzi Katika Nyimbo Za Wasanii Teule ................65
4.4.1 Tija Zipatikanazo .............................................................................................65
4.4.1.1 Kuburudisha jamii ..........................................................................................65
4.4.1.2 Kudumisha Mahusiano ...................................................................................66
4.4.1.3Kukuza Msamiati wa Lugha ...........................................................................66
4.4.1.4 Kuelimisha Jamii ............................................................................................67
4.4.2 Madhara ya Nyimbo Zenye Vionjo vya Mapenzi ............................................67
4.4.2.1 Kujiingiza Katika Mahusiano ya Umri Mdogo ..............................................67
4.4.2.2 Mmomonyo wa Maadili Katika Jamii ............................................................68
4.4.2.3 Kudumaza kwa Ubunifu .................................................................................68
4.4.2.4 Ufinyu wa Mawanda .......................................................................................69
4.5 Muhtasari wa Sura ya Nne ....................................................................................69

**SURA YA TANO: MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO ..........70**
5.1 Utangulizi ..............................................................................................................70
5.2 Muhtasari wa Tasnifu ............................................................................................70
5.3 Mapendekezo kwa Tafiti Zijazo ...........................................................................70
MAREJELEO ...........................................................................................................72
VIAMBATISHO .......................................................................................................75
A. NYIMBO ZA MAPENZI KUTOKA KWA WASANII TEULE .........................75
KIAMBATISHO 1 ....................................................................................................75

A.1 Nyimbo za Mwanafalsafa .....................................................................................75
A.1.1 “Mi na Mabinti” – Mwanafalsafa .....................................................................75
B:MIONGOZO YA UDODOSAJI NA USAILI.......................................................79
B: Mwongozo wa Usaili kwa Wataalamu kutoka BAKITA/TATAKI, Wanamuziki wa zamani, Watayarishaji wa muziki. ..........................................................................79
B:2 Mwongozo wa usaili kwa Watu wazima wenye umri wa miaka arobaini na kuendelea ...............................................................................................................81
B:3 Mwongozo wa Mjadala wa vikundi kwa vijana wenye umri wa miaka (15-35).82

## ORODHA YA VIFUPISHO

### Maneno Yaliyotumika na Maana zake

B F: Bongo Fleva

BAKIZA: Baraza la Kiswahili Zanzibar

Inspekta: Haruna Kahena

Mwana FA: Mwanafalsafa

Mwanafalsafa: Hamisi Mwinyijuma

R & B: Rhythm and Blues

TUKI: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili

# SURA YA KWANZA

# UTANGULIZI

## 1.1 Usuli wa Tatizo la Utafiti

Mapenzi ni dhana pana ambayo imewashughulisha watu wenye taaluma mbalimbali na ujuzi tofauti katika kuielezea kwa namna tofauti. Aghalabu, msamiati huu hutumika kuelezea hisia nzito ya moyoni inayomfanya mtu avutiwe, athamini na ajali mtu, kitu au jambo; mahaba, huba (BAKIZA, 2010).

Kwa mujibu wa TUKI (2004), mapenzi ni hali ya kuingiwa moyoni na kumthamini mtu au kitu zaidi ya mwingine au kingine. Suala la mapenzi linakwenda sambamba na upendo hivyo ni vigumu kuzitenga dhana hizi. Suala la mapenzi katika jamii zetulinaonekana kuchukuliwa kwa uzito wapekee fulani. Hii inadhihirishwa na jinsi ambavyo suala hili linavyojadiliwa au kuzungumziwa hata katika maeneo ya biashara ambayo hayana uhusiano wa moja kwa moja na mambo ya mapenzi. Ponera (2015) anasema;

> "Kwa jamii za Afrika Mashariki, mapenzi na ngono huchukuliwa kwa namna tofauti na jinsi linavyochukuliwa na jamii nyinginezo; mathalani, jamii za Afrika Magharibi. Vipengele mbalimbali vya kimaisha kama vile mazungumzo, utani, ngomezi, ngoma, bembezi, dansi, taarabu (maudhui ya nyimbo pamoja na fani ya uchezaji wake) na sanaa nyinginezo za wanajamii wa Afrika Mashariki hufanywa kwa kuelezwa katika eneo la katikati ya miili (fikra za ngono)." (Uk. 15)

Lugha ni zana muhimu sana katika mawasiliano ya kila siku baina ya mtu na mtu. Lugha hutoa mchango mkubwa katika maisha ya kila siku. Mathalani, lugha kwa kiasi kikubwa ilitoa na inaendelea kutoa mchango katika kufundisha na mchakato

mzima wa ujifunzaji (Senkoro, 2003). Usawiri wa uzungumzwaji wa masuala ya mapenzi katika tanzu mbalimbali za fasihi katika jamii ya sasa si jambo geni, kwani wasanii wengi wa fasihi kwa ujumla wamekuwa wakitumia lugha ambayo huweka bayana masuala ya mapenzi, tena bila ya kificho katika kazi zao. Hata hivyo, kuzungumzwa kwa suala hili la mapenzi waziwazi bila ya kificho kumesababisha madhara makubwa katika jamii zetu. Miongoni mwa madhara hayo ni kuporomoka kwa madili yetu, kukiukwa kwa mila na desturi za Tanzania. Suala hili limesababisha watoto na vijana kujiingiza katika masuala ya mapenzi na kujamiiana katika umri mdogo, na hata kuwa katika hatari ya kupata maradhi ya ngono na UKIMWI na vifo katika umri mdogo. Licha ya hivyo, jamii ya sasa imebadilika kwa kiasi kikubwa tofauti na jamii ya kizazi kilichotangulia cha wazee wetu. Wakati huo mambo yahusuyo mapenzi yalikuwa ni ya kificho sana. Na haikuwa rahisi kwa vijana kufahamu masuala yahusuyo hayo kabla ya kufikia umri wa kwenda jando[1] na unyago[2] au hata kabla ya kuingia katika ndoa. Kutokuwapo kwa shughuli hizo kwa jando na unyago katika jamii ya sasa kuna athari kubwa zikiwemo, mmomonyoko wa maadili na kuwafanya wasanii wa muziki wa kizazi kipya kuimba nyimbo zilizobeba dhana za mapenzi na mahusiano kama ni jambo la kawaida sana.

Omari (2006) anaelezea harakati za vijana wa Zanzibar dhidi ya utamaduni kupitia muziki wa Bongo Fleva. Anazungumzia namna vijana wa Tanzania Visiwani walipoanza kujihusisha na muziki huu, jinsi ulivyopokewa mnamo miaka ya 1980 ukikinzana na masuala ya kiutamaduni pamoja na changamoto zake katika jamii hiyo ya Wazanzibar. Omari ananukuu Perullo (2007:252) akisema kuwa siku za

[1] Jando ni sherehe/shughuli ambazo vijana wa kiume hupelekwa kwa lengo la kutahiriwa na kufundishwa maadili mema na namna ya kulea mke na familia kwa ujumla.
[2] Unyago ni shughuli/sherehe ambazo hufanyiwa vijana wa kike mara baada ya kuvunja ungo/kubalehe. Huko hufunzwa namna ya kumtunza mume, masuala ya mahusiano, kujitunza na kuwa msafi pamoja na namna ya kulea familia yake baadaye atakapoolewa.

mwanzoni maendeleo ya muziki wa rap katika visiwa vya Zanzibar ilikuwa ni tofauti na Tanzania Bara. Mathalani, anamnukuu *DJ Salehe* anayesema kuwa vijana walianza kwa kuiga nyimbo za rap za Marekani kwa lugha ya Kiingereza. Kwa kipindi hiki, katika Visiwa vya Zanzibar hakukuwa na vyombo vya habari vya watu binafsi ila kulikuwa na kituo cha redio kilichokuwa kinamilikiwa na serikali kilichojulikana kama Sauti ya Tanzania Zanzibar (STZ) na Televisheni ya Zanzibar (TVZ) vyombo hivyo vyote vya habari vilikuwa haviupigi muziki wa *Bongo Fleva* kwani muziki huu ulikuwa unahusishwa na uhuni na hata wale vijana waliokuwa wakiimba muziki huu walionekana wamepotoka na kuonekana ni wahuni wasiofaa katika jamii.

Vilevile, muziki wa Bongo fleva ulikuwa unaonekana ni muziki ambao unaeleza mambo kwa uwazi zaidi, haufichi mambo kama ilivyozoeleka katika ngoma za asili za kiutamaduni kama vile Msewe au Uringe ambazo zote zinapatikana visiwa vya Zanzibar, waliendelea kusema kuwa siku hizi vijana wanapokuwa wanacheza muziki huu wanacheza kwa ukaribu sana, hakuna mipaka baina ya wanaume na wanawake kama ilivyokuwa imezoeleka awali hivyo muziki huu huweza kusababisha kujiingiza katika masuala ya uasherati.

Kwa Zanzibar, baadhi ya kizazi cha watu wazima waliuhusisha muziki wa Bongo Fleva na utamaduni wa nje. Vipengele vya namna ya uvaaji (mavazi yao) na namna ya uchezaji havikukubalika. Hii ilitokana na imani za kidini na za kiutamaduni. Hivyo, jambo la busara ilikuwa ni kuupinga muziki huu kwa namna yoyote ili kuweza kunusuru shughuli za kiutamaduni ambazo zimehifadhiwa na jamii kwa muda mrefu.

Kwa miaka mingi, muziki wa hip hop umevuta hisia za watu na waandishi wengi ulimwenguni kote kutokana na kuenea kwa kasi (Reuster-Jahn, 2007). Hii ni kutokana na kuwa toka kuibuka kwake umekuwa unaelezea hali halisi ilivyo katika jamii masuala ya siasa, uchumi, mapenzi na matatizo wanayoyapata wanajamii. Utafiti uliofanyika juu ya utanzu huu umechunguza njia mahususi za namna hip hop ilivyoenea, ilivyopokewa ilivyoendelezwa na mabadiliko iliyoyapata katika mazingira tofauti (Kraidy, 1999; Frimpong, 1999).

Lugha inayotumika katika tungo zinazoelezea suala la mapenzi katika muziki wa kizazi kipya bado haijashughulikiwa vya kutosha na wataalamu na wanafasihi ya Kiswahili. Kwa mfano, Majembe, Fenn na Perullo (2000) waliangalia suala la kuchanganya lugha, hasa Kiingereza na Kiswahili, katika muziki wa hip hop. Chachage (2002) anawakosoa wenye mawazo potofu juu ya muziki wa hip hop na Omari (2009) anachambua mitindo ya lugha ya ushairi inavyotumika katika muziki wa hip hop (yeye akiuita muziki wa bongo fleva). Almas (2011) anajadili mchango wa hip hop katika kukuza lugha ya Kiswahili. Sanga (2011) naye aliandika kuhusu usawiri wa mwanamke katika muziki wa kizazi kipya. Wengine waliojishughulisha na jambo hili ni Mangesho (2003) na Senkoro (2003).

Hoja zilizotusukuma kufanya utafiti kuhusiana na matumizi ya lugha inayotumika katika tungo za mapenzi muziki wa kizazi kipya ni hizi; Mosi, ni kwamba muziki huu wa kizazi kipya, kwa sasa ni miongoni mwa nyanja muhimu ambayo inatumiwa na wanajamii katika kuzungumzia masuala mbalimbali yanayoihusu jamii husika. Mambo hayo ni kama vile maafa na shida mbalimbali zinazowakabili, masuala ya kisiasa kutoa elimu juu ya masuala tofauti. Lugha ya kuwasilisha maudhui yaliyokusudiwa haina budi kuzingatia muktadha, rika, mada ya mazungumzo pamoja

na uelewa wanaofikishiwa ujumbe huo. Pili ni mtazamo mtafiti juu ya muziki huu wa kizazi kipya. Mtafiti ana mtazamo chanya kuhusu muziki huu. Hii ni kwasababu licha ya kuelimisha na kuburudisha jamii, pia, umekuwa chanzo cha ajira kwa vijana pamoja na kuwa chanzo cha mapato kwa serikali. Kama tu itaamua kuwekeza na kudhibiti uharamia wa kazi za wasanii. Na, tatu ni hali ya kutokuwapo kwa utafiti wa kina uliowahi kufanywa juu ya matumizi ya lugha katika muziki wa kizazi kipya hususani tungo za mapenzi zinavyoweza kuibua misimu mbalimbali ya lugha ya Kiswahili.

## 1.2 Tamko la Tatizo la Utafiti

Sehemu kubwa ya wachunguzi wa fasihi, wataalamu wa lugha, pamoja na watu wazima wenye umri wa kuanzia miaka arobaini na kuendelea wamekuwa na mtazamo tofauti juu ya muziki wa kizazi kipya. Huona kuwa ni muziki wa usio na maadili kwa jamii, na hata kudiriki kuita aina hii ya muziki kuwa ni muziki wa kihuni au muziki wa wahuni ( Mangesho, P 2003). Miongoni mwa vipengele vinavyosababisha hali hiyo ni matumizi ya lugha muziki huu hutumia tamathali za semi, lugha ya picha na ishara. Mara nyingi, vipengele hivyo huwa ni vya wazi mno kiasi cha kushindwa kufumba masuala mbalimbali, hususani, yale yanayohusu mapenzi, yanayomjadili mwanamke pamoja na sehemu ya viungo vya mwili. Hii huwa kama sehemu ya wimbo kuona na ndiyo desturi na asili ya muziki huu (Mbughuni, 1982; Momanyi 2001). Jambo hili hujidhihirisha katika tungo za muziki wa kizazi kipya, hususani, zile za wasanii wa awali na wa kipindi cha sasa.

Namna uchambuzi wa kazi za fasihi unavyofanyika, si tu umeendelea kutoa picha na rai zenye mtazamo hasi juu ya matumizi ya lugha katika muziki huu, bali pia unashindwa kuonesha hali halisi ilivyo juu ya lugha inavyotumika, sababu za kutumia

maneno, misamiati hiyo na namna wanavyoibua misimu[3] tofauti ya lugha katika jamii hususani katika tungo za mapenzi. Utafiti huu unalenga kuangalia kwa undani jinsi matumizi ya lugha ya muziki wa kizazi kipya, hususani tungo za mapenzi za wasanii tajwa jinsi ulivyotumika na kutofautiana na tungo zisizokuwa za mapenzi. Kipengele cha uteuzi wa misamiati/maneno kimeangaliwa zaidi ili kuweza kuona namna tungo hizo zilivyojipambanua katika matumizi ya lugha.

## 1.3 Malengo ya Utafiti

### 1.3.1 Lengo Jumla

Kuchunguza lugha inayotumiwa na wasanii wa muziki katika tungo zinazozungumzia dhana ya mapenzi katika muziki wa kizazi kipya.

### 1.3.2 Malengo Mahsusi

a) Kubainisha lugha inayotumika kusawiri vionjo vya kimapenzi katika nyimbo za wasanii teule wa muziki wa kizazi kipya;

b) Kuchunguza sababu zinazowafanya wasanii teule kutumia lugha hiyo katika kusawiri vionjo vya kimapenzi katika nyimbo zao, na;

c) Kuchunguza athari ambazo hadhira hupata kutokana na matumizi ya nyimbo zinazobeba dhana ya mapenzi katika jamii.

[3] Misimu – ni maneno mbayo huibuliwa na kikundi fulani cha jamii hukutumika kwa kipindi fulani kisha hutoweka pindi yanapokosa mashiko. Maneno yanayodumu husanifishwa na kutumika kama Kiswahili sanifu. Miongoni mwa misimu iliyodumu ni kama vile Fisadi, uchakachuaji, bongo, daladala na mengineyo.

## 1.4 Maswali ya Utafiti

a) Je, ni lugha ipi inayotumika katika kusawiri vionjo vya mapenzi katika nyimbo za wasanii teule wa muziki wa kizazi kipya?

b) Je, ni sababu zipi zinazowafanya wasanii teule wa muziki wa kizazi kipya kutumia lugha hiyo katika kusawiri vionjo vya kimapenzi katika nyimbo zao?

c) Je, ni athari zipi ambazo hadhira huzipata kutokana na matumizi ya lugha katika nyimbo zinazobeba dhana ya mapenzi katika jamii?

## 1.5 Manufaa ya Utafiti

Mosi, ni kusaidia kuzichambua nyimbo za wasanii wa muziki wa kizazi kipya ili kuzielewa na kubanisha ubora wa lugha katika tungo hizo na makusudio ya wasanii kuzitumia dhana hizo katika tungo zao. Pili, wasomaji wa tasnifu hii watapata fursa ya kujua mtazamo wa wasanii hawa juu ya dhana ya mapenzi, huku wakihusisha na matumizi ya lugha katika tungo hizo. Tatu, tasnifu hii imekuwa ni chachu kwa wataalamu ili kuangalia kwa jicho pevu mapengo yaliyopo katika utafiti na kuchunguza kwa makini ubora wa lugha inayotumika katika tungo zinazoelezea masuala ya mapenzi na mahusiano katika muziki wa kizazi kipya. Nne, ni kuondoa dhana iliyoenea katika jamii, hasa kwa watu wazima na viongozi wa dini na serikali, kuwa muziki wa kizazi kipya ni wa kihuni na unawahusu wahuni; hivyo, hauna mchango wala faida yoyote katika jamii. Tano, kusaidia kuhifadhi baadhi ya nyimbo za wasanii teule.

### 1.6 Taarifa Fupi za Wasanii Teule

#### 1.6.1 Taarifa Fupi ya Inpekta Haroun

Jina lake kamili anaitwa Haruna Kahena ni mzaliwa wa Temeke Mikoroshini, wilaya ya Temeke mkoa wa Dar es Salaam. Ni baba wa watoto watatu na mke mmoja anayetambulika kwa jina la Sada bint Shabani ambao walifunga ndoa toka mwaka 2004 na kujaliwa watoto hao watatu, wa kiume wawili na wa kike mmoja. Elimu yake ni kidato cha pili kwani alishindwa kuendelea na masomo kutokana na matatizo ya kiuchumi yaliyoikumba familia yake. Mara baada kuacha shule alianza kujishughulisha rasmi na shughuli za muziki licha ya kuwa kuimba alianza toka alipokuwa yupo shuleni. Walikutana na msanii mwenzake Karama Rashidi (Luteni Karama) katika moja ya matamasha yaliyokuwa yanaandaliwa na vituo vya redio kwa lengo la kuibua vipaji katika ukumbi uliokuwa unajulikana kwa jina la FM Club uliopo Kinondoni na kuunda kundi la “Gangwe Mobb”. Kwa pamoja waliunda kundi hilo na kufanikiwa kutoa nyimbo nyingi ambazo ziliwahi kutamba katika vituo mbalimbali vya redio ikiwemo “Mtoto wa Geti Kali”, “Pamba Nyepesi”, “Haina Kulemba”, “Nje Ndani” na nyinginezo. Kwa sasa Inspekta masuala ya muziki kidogo ameyaweka pembeni, anafanya mara chache kwani ameamua kujikita zaidi na shughuli zake za biashara.

#### 1.6.2 Taarifa Fupi ya Mwanafalsafa

Jina lake kamili anaitwa Hamisi Mwinjuma ni mtoto wanne katika familia ya watoto watano wa mzee Alfani Mwinjuma ambaye alikuwa mtumishi wa serikali. Mama yake mzazi alitambulika kwa jina la Mwansiti bint Mtoro. Kiasili Mwanafalsafa ni mdigo wa wilaya ya Muheza mkoa wa Tanga kwa baba na mama yake. Mtoto wa

kwanza katika familia ya mzee Alfani Mwinjuma, anaitwa Aisha, wa pili Mohamedi (*China Black* ) wa tatu anaitwa Kassimu (*Kasir),* wa nne ndio Khamisi Mwinjuma(Mwanafalsafa) na mtoto wa mwisho ni Mariamu. Kaka zake Mwanafalsafa nao waliwahi kujihusisha na shughuli za muziki wakati wanasoma shule ya msingi Mnazi Mmoja kipindi wazazi wao walipohamishiwa Dar es Salaam kikazi kundi la kaka zake Mwanafalsafa walipokuwa shuleni liliitwa Quite Gangster (1987 – 1990)

Mwanafalsafa alianza shule ya msingi mnamo mwaka 1986 – 1993 katika shule ya msingi Mdote iliyopo wilaya ya Muheza mkoa wa Tanga na baadae sekondari miaka ya 1994 – 1997, kidato cha tano na sita miaka ya 1998 – 2000. Baadae elimu ya juu kwa kiwango cha advance diploma ya Marketing katika Chuo cha Usimamizi wa Fedha (IFM) na baadaye alipata shahada ya pili ya uzamili Master in Finance huko Uingereza katika chuo cha Durham University. Kwa sasa Mwanafalsafa ana mchumba ambaye wamejaliwa kupata mtoto mmoja wa kike. Tofauti na shughuli za sanaa za uimbaji yeye aliwahi kuwa mtumishi wa benki ya biashara ya NBC idara ya bima (Insuarance) mpaka mwaka 2010 alipomaliza mkataba na benki hiyo na kuamua kufanya shughuli zake binafsi.

## 1.7 Nadharia Iliyotumika Katika Utafiti

### 1.7.1 Misingi ya Nadharia ya Umuundo

Nadharia ya Umuundo inahusishwa na wana-isimu wa mkondo wa fikra wa Prague ambao walihusika na Urasimi wa Kirusi kabla ya kuanguka kwake. Kuzuka kwa mkondo wa fikra wa Prague kulihusiana kwa kiasi kikubwa na urasimi, hasa wale wa kikundi cha wana-isimu wa Moscow ambao waliathiriwa na mawazo ya wahakiki wa

kirasimi wa nchi za Chekislovakia (Herbatian Formalism). Wana-umuundo huchunguza muundo wa ndani wa kazi za kifasihi, hasa za kishairi ambazo walishughulika nazo zaidi. Katika hatua za mwanzo, wahakiki kama Roman Jakobson (1896 - 1982) walivutiwa na kiwango cha sauti katika ushairi. Naye Jan Mukarovsky (1891 - 1975) alilichunguza zaidi suala la mizani katika ushairi wa ki-Chekislovakia. Wahakiki hawa baadaye waliichunguza sanaa wakilinganisha na hali za kijamii pamoja na jinsi kazi za kifasihi zinavyoashiria uhalisi nje ya mawanda ya lugha (Wamitila, 2002).

Lengo kuu la wana-Umuundo lilikuwa ni kurejesha uhakiki kwenye uchunguzi wa kazi za fasihi kama Uhakiki Mpya. Lakini wana-Umuundo waliamini kuwa haiwezekani kuichunguza kazi ya fasihi bila ya kuwa na mawazo au chukulizi fulani kabla ya kuanza uchunguzi huo (Wamitila, 2002). Aghalabu, umuundo ni nadharia inayohusiana sana na kutafsiri matini kwa kuzingatia miundo inayojenga kazi. Umuundo hujishughulisha zaidi na uhusiano wa vionyeshi, yaani, maneno yenyewe na dhana inayorejelewa na neno kama vile vitu, hali na mambo yanayooneshwa. Nadharia hii inapinga wazo la kijadi linalodai kwamba fasihi ni tokeo la mchango wa fani na maudhui. Dhana ya kimapokeo ya kifasihi inasemekana ni umbo lenye viungo viwili ambavyo ni maudhui na fani yawezekana kwa viungo hivi kutenganishwa (Njogu, 2007). Muundo unafananishwa na mtindo ukimaanisha lugha inayotumika katika maandishi au mazungumzo ya kifasihi (Leech & Short, 1981). Kifasihi, mtindo huelezwa kwa kubanishwa na madhumuni ya msanii. Madhumuni ni dhamira na mtindo ni jinsi dhamira zinavyowasilishwa. Hivyo basi, wanamuundo wanaamini kuwa kwanza mtu huanza kuwa na wazo katika fikra za msanii au msemaji yeyote wa kifasihi. Jukumu la mwanasanaa ni kuainisha na kutumia lugha inayofaa katika kulieleza wazo hilo.

Mwanaisimu Ferdinand de Saussure alidai kuwa lugha ina sehemu kuu mbili zinazojidhihirisha katika usemaji. Sehemu hizo ni: Mosi, ni kuwa kuna lugha inayojikita katika maongezi ya kila siku, yaani, lugha dhahiri. Pili, kuna lugha dhahania – hii ni ile ambayo daima haibainiki wazi, ijapokuwa baadhi ya kanuni zake huthibitika katika maongezi ya kila siku. Kutokana na fikra hii, De Saussure alisema kwamba lugha dhahiri au lugha tumizi huonyeshwa katika uwezo wa mtu kuunda idadi ya sentensi kadiri anavyotaka.

Umuundo unaiona lugha kuwa ni nguzo ya msingi wa kufafanua viungo vyote vinavyotumika pamoja kuunda kielelezo cha kisanaa kinachokusudiwa kutumika kuelezea jambo kwa ajili ya jamii. Lugha ndiyo mhimili unaoviunganisha na kuvioanisha viungo vyote vya fasihi kuwa kitu kimoja. Ukusanyaji wa data na uchambuzi wa data na uwasilishaji wake utafanywa kwa kuzingatia mhimili wa nadharia hii ambao ni lugha katika viwango mbalimbali vya fonolojia, sintaksia na semantiki.

Misingi ya nadharia hii ya Umuundo ni;

a) Wanamuundo walichunguza muundo wa ndani wa kazi za fasihi, hasa ushairi. Walianza na sauti baadae mizani, licha ya hivyo, pia waaliangalia sanaa kwa kulinganisha na hali za kijamii, na jinsi kazi za fasihi zinavyoashiria uhalisi uliopo nje ya mawanda ya lugha. Kwa kutumia hoja ya msingi huu ilitusaidia kufikia lengo mahususi la kwanza ambapo ni kubainisha lugha inayotumika kusawiri vionjo vya mapenzi katika tungo hizo
b) Mawazo ya Ferdinand de Saussure yanasaidia sana katika kuuweka msingi wa umuundo kwani yeye alitofautisha kati ya matendo ya ki-usemi/kauli'*parole*' na mfumo mpana wa lugha*'langue'*. Anaona tamko

lolote huwa na maana linapoangaliwa katika mfumo mpana wa lugha. Vilevile, aliielezea lugha kuwa ni mfumo wa ishara ambazo huungana na kuunda mkufu mkubwa wa ishara; ambapo, kila ishara huwa na sehemu mbili kuu *parole* na *langue*. Uhusiano wa kiashiria na kiashiriwa huwa ni wa kinasibu tu.

c) Wanamuundo wanaamini kuwa fasihi huangaliwa kama njia fulani maalumu ya utumiaji wa lugha; na kwa njia hiyo, ikapata sifa ya kuitwa lahaja ya kiuamilifu '*active dialect'*. Misingi mingine ya nadharia hii ya muundo itatuongoza kufikia lengo mahususi la pili linalohusu sababu za kutumia lugha hiyo na lengo mahususi la tatu linalohusu athari ambazo hadhira hupata kutokana na matumizi ya nyimbo zinazobeba dhana za mapenzi katika jamii.

d) Wanamuundo pia wanaamini kuwa lugha ya kishairi ni tofauti na lugha ya kawaida kutokana na sifa ya kuzichimuza ishara za lugha. Walichunguza upatanishi wa sauti, kiimbo, arudhi na utunzi wa mashairi, wakabaini kuwa kazi ya fasihi ina mpangilio wa viwango mbalimbali: *kiwango cha sauti, kiwango cha wizani, kiwango cha sarufi*, n.k. Mhakiki anaweza kuchunguza kiwango fulani tu, au zaidi ya kimoja, au viwango mbalimbali kwa jumla.

e) Wanamuundo wa mwanzo waliamini kuwa haiwezekani kuichunguza kazi ya fasihi bila ya kuwa na mawazo (chukulizi) fulani kabla ya kuanza uchunguzi huo. Lakini wana uhakiki mpya, waliamini kuwa mhakiki sharti ajifungie kwenye kazi ya fasihi bila ya kujihusisha na kitu kingine kilicho nje. Kwa hiyo, uchukulizi '*suppositions/assumptions'* haukuwa na nafasi kwao.

### 1.7.2 Jinsi Nadharia Hii Ilivyotumika

Tulitumia nadharia hii ya umuundo katika kuchunguza muundo wa ndani wa mashairi ya nyimbo hizo za mapenzi za Inspekta Haroun na Mwanafalsafa. Muundo huo wa ndani ulilinganishwa na hali za kijamii, na jinsi nyimbo hizo zinavyoashiria uhalisi katika jamii nje ya mawanda ya lugha. Vilevile, nadharia hii ilituongoza kuangalia nyimbo hizo kama njia maalumu ya utumiaji wa lugha na kuwa na sifa ya kuitwa lahaja ya kiamilifu. Pia, nadharia ilituongoza kuonesha kuwa lugha ya kishairi ni tofauti na lugha ya kawaida kutokana na kuwa na sifa za kuzichimuza ishara za lugha katika matumizi ya lugha yalivyotumika na jinsi lugha ilivyobeba ishara fulani.

## 1.8 Muhtasari wa sura ya kwanza

Sura hii imeangalia mambo mbalimbali yanayohusiana na utafiti wetu. Nayo ni usuli wa tatizo la utafiti, tamko la utafiti, malengo ya utatifi huu, na manufaa yake kwa jamii na wanataaluma. Pia, imeelezwa namna nadharia ya Umuundo na mwisho. Masuala ya mapitio ya maandiko kuhusiana na mada ya utafiti yameelezwa katika Sura ya Pili.

# SURA YA PILI

# MAPITIO YA MAANDIKO

## 2.1 Utangulizi

Sura hii inabainisha mapitio mbalimbali yanayohusu muziki wa kizazi kipya. Mapitio hayo yanatoa mwanga juu ya mtazamo wa matumizi ya lugha ya muziki wa kizazi kipya, hususani, tungo za mapenzi. Sura hii ina jumla sehemu tatu. Sehemu ya kwanza inahusu machapisho yanayozungumzia chimbuko na maendeleo ya muziki wa kizazi kipya. Sehemu ya pili machapisho yanayoelezea matumizi ya lugha na muziki wa kizazi kipya. Mwisho ni mapengo yanayopaswa kuzibwa.

## 2.1 Maandiko Kuhusu Chimbuko na Maendeleo ya Muziki wa Kizazi Kipya

Muziki wa kizazi kipya ni aina ya muziki wenye mahadhi ya mchanganyiko wenye vionjo vyenye asili ya Caribean na Amerika na sehemu nyingine duniani. Nchini Tanzania, muziki huu uliingia mnamo miaka ya 1980-1990 ambapo waimbaji wake waliimba kwa kuchanganya lugha ya Kiingereza na Kiswahili na hata kutumia ala za muziki wa kigeni (Muziki wa Ki-Amerika). Aina nyingine ya muziki wa kizazi kipya ni kama vile zuku '*Zouk',* rumba, *Hip hop*, nk muziki ulikuwepo Tanzania kipindi hiki ni ule muziki wa dansi wa akina Marijan Rajab, Mbaraka Mwinshehe na wengineo.

Vilevile muziki wa kizazi kipya unaweza kuelezwa kama ni shirikisho la tanzu mbalimbali za muziki ambazo ni mashuhuri kwa maana ya kupendwa na kusikilizwa na idadi kubwa ya watu nchini Tanzania. Baadhi ya tanzu hizo ni hiphop (muziki wa kufokafoka), *R&B* (muziki wa mahadhi ya taratibu), zuku, mchiriku na mengineo.

Aina hii ya muziki uliingia katika jamii ya Watanzania mwishoni mwa mwaka 1970 na kushika kasi miaka ya1980. Utandawazi ndio chanzo kikubwa cha kuibuka kwa muziki huu. Chimbuko la Muziki huu wa kizazi kipya kimsingi unahusishwa na *"popular music*" muziki maarufu/mashuhuri ambao nao ni tokeo/kipengele kimojawapo cha *"Popular culture"* utamaduni mashuhuri.

Muziki huu wa kizazi kipya wengine wanautambua kama muziki wa hip hop au muziki wa bongo fleva kuingia kwake nchini Tanzania kumeelezwa kwa namna tofautitofauti. Baadhi ya wataalamu kama vile (Chachage, 2002; Mangesho, 2003) wanaona kuwa chimbuko la muziki huu ni mwanzoni mwa miaka ya 1980 na mwanzoni mwa miaka ya 1990. Wengine kama vile Perullo (2003), Omari (2006) na Jilala (2008) wanaona kuwa muziki huu ni fasihi pendwa ambayo inakua kila siku na kupata wafuasi wengi ambao ama ni wanamuziki au ni mashabiki wa muziki huu.

Hapo awali, neno hili la 'bongo' nchini Tanzania lilikuwa likitumika kurejerea jiji la Dar es salaam, jiji ambalo inaaminika ili mtu aweze kuishi na kustahimili maisha ya mji huu hana budi kutumia ubongo ndipo aweze kufanikiwa kimaisha. Baadaye, mnamo miaka ya 1990 katikati hali ilbadilika na neno bongo likawa linatumika kurejelea nchi nzima ya Tanzania (Suriano, 2007:207). Fleva ni neno lenye asili ya lugha ya Kiingereza ambalo limetoholewa huko '*Flavour'* likiwa na maana ya ladha (Englert, 2003:75) wakati bongo fleva kwa ujumla ni neno lililorejea maana ya '*Tanzania tastes'* au ladha ya muziki wa Kitanzania (Mangesho, 2003 na Omari, 2009). Mwanzoni, vijana walianza kwa kuimba muziki huu wakiwa ufukweni na baadaye katika sherehe mbalimbali za wanafunzi mashuleni ambazo ziliandaliwa na wanafunzi wenyewe. Sherehe hizo ni kama vile za kuwaaga na kuwakaribisha

shuleni kwa ngazi tofauti ya elimu ya sekondari. Muziki huu kusikika kwenye vyombo vya habari kama vile redioni ulianza mwaka 1995.

Kwa kipindi cha awali, muziki huu ulitawaliwa na ujumi[4] mwingi wa kimagharibi katika vipengele vya fani na maudhui. Kadri miaka ilivyoenda mambo hayo yalibadilika na muziki huu ukaanza kuelezea ujumi wa Waswahili wenyeji na kuufanya kuwa na sifa za kipekee. Vijana wa Kitanzania waliutumia muziki huu kwa ajili ya kuelezea matatizo yao ya kila siku. Matatizo hayo kama vile ukosefu wa ajira na athari zake, dola na mambo yake, masuala ya mahusiano ya kimapenzi, masuala ya siasa na mengineyo.

Chachage (2003:23) naye amejadili kuhusiana na asili ya muziki huu wa kizazi kipya, ambapo, yeye anadai kuwa Hip hop na R&B asili yake ni mwingiliano wa tamaduni nyingi zikiwemo za kiafrika. Muziki huu ni sehemu ya utamaduni wa ukinzani duniani. Utofauti unaojitokeza katika aina hii ya muziki huu wa Tanzania na ule wa Marekani kwa sasa ni fani na maudhui yake, ijapokuwa misingi inafanana. Hawa vijana wanakataa kuisherehekea hii mipaka ya nchi iliyowekwa na akina Bismarck[5] 1884 na kungana kiutamaduni na watu wengine wenye asili ya Afrika popote pale wanapoonewa. Hivyo basi utanzu huu wa fasihi kwa kiasi kikubwa sifa yake katika jamii umepewa nafasi katika kuelezea hisia na matakwa ya vijana, lakini zaidi katika kufichua maovu na ukandamizwaji wa kimfumo bila ya kujali taratibu na kanuni kandamizi zilizopo (Askew, 2002).

---

[4] Ujumi ni tawi la kitaaluma la kifalsafa linalojishughulisha na dhana ya uzuri wa kitu au kitu kizuri,mtu, asili na sanaa kwa kwa kuhusisha ukomavu wa hisia akilini, muono, wazo, desturi, idili na uhalisi wa jamii maalum.

[5] Bismarck – alikuwa waziri mkuu wa Ujerumani miaka ya 1880s ambaye aliitisha mkutano mkuu wa Berlin kwa lengo la kuligawa bara la Afrika kwa wazungu.

Hapo zamani nyimbo ziliimbwa kwa kuwaiga wasanii wa Kimarekani kuanzia lugha hadi maudhui. Kwa mfano, Saleh Jabir mwanzoni mwa miaka ya 1990 katika kanda yake iitwayo *Swahili Rap* alitumia mapigo ya muziki wa wasanii wa Kimarekani kama vile *Vanilla Ice, Kriss Kross* na *Naught by Nature*. Hali kadhalika walitumia baadhi ya maneno na sentensi kutoka katika mashairi ya nyimbo hizo (Remes, 1998:320).

Hivyo basi, muziki wa bongo fleva (Kizazi kipya) kwa kiasi kikubwa ni muziki ambao unabadilika kulingana na wakati (Raab, 2006:19, Perullo na Fenn, 2003:2) kwani hapo awali muziki huu kwa kiasi kikubwa ulikuwa umetawaliwa na vionjo vya *hip hop* ya Amerika. Kwa sasa, Bongo fleva inajumuisha mitindo tofauti ya muziki kama vile muziki wa kufoka (*Hard-core rap*) mpaka muziki laini, taratibu na ule wa zuku (*Zouk*) na '*Blues' (Rhythm & Blues*) huku nyimbo nyingi kwa kiasi kikubwa zikihamasisha na kuendeleza muziki wa kitanzania na tanzu zake kama vile ngoma, dansi, taarabu, mchiriku na nyinginezo.

Kwa mujibu wa Perullo (2003:49), Bongo fleva ni msamiati unaotumika kuelezea muziki wa kigeni ambao umechukua na kutumia mapigo ya asili. Ijapokuwa jambo la msingi la kuzingatia hapa ni kuwa hapo awali muziki wa kigeni ulikuwa unatumia lugha mapigo ya asili lakini muziki huo haukuwa ukitambulika kama muziki wa Bongo fleva. Hivyo basi, maendeleo ya muziki wa *hip hop* kwa Tanzania hayapo tu katika kuutambulisha utamaduni na tasnia ya muziki pekee bali hata kwa manufaa na maendeleo ya fasihi ya Kiswahili.

Muziki wa kizazi kipya (Bongo fleva) kwa kiasi kikubwa huelezea hali halisi ya maisha ya kijamii, mathalani wasanii hutoa maoni yao kuhusu siasa, rushwa, na hali ngumu za maisha zinazowakabili watu na jamii kwa ujumla. Pia Bongo fleva ina jukumu kubwa la kuelimisha jamii (Englert, 2003).

## 2.2 Maandiko Kuhusu Matumizi ya Lugha na Muziki wa Kizazi Kipya

Kahigi (1995) anazungumzia lugha inayotumika katika vitabu vya watoto namna inavyoweza kukizi haja ya wahusika hao na mambo ya kuzingatia katika kubainisha lugha za vitabu vya watoto. Utafiti huu wa Kahigi unahusiana na utafiti wetu kwa kiasi fulani; yumkini, yeye alijikita zaidi kujua matumizi ya lugha kulingana na mahitaji maalumu ikiwemo rika jinsia na kadharika, wakati utafiti wetu unajikita katika kuchunguza matumizi ya lugha katika muziki wa kizazi kipya hususani tungo za mapenzi za wasanii teule.

Songoyi (2005) amewahi kufanya uchunguzi kuhusiana na suala la miundo na maudhui ya nyimbo za Kisukuma. Katika kazi yake amedhirisha kuwepo kwa suala la matumizi ya lugha katika fasihi simulizi ya Wasukuma kama ilivyo katika fasihi simulizi ya makabila mengine yanayopatikana nchini Tanzania na duniani kwa ujumla. Anabainisha kuwa kipengele hiki cha matumizi ya lugha hujidhihisha katika aina za utani na watani wa Kisukuma. Ameongezea kuwa tofauti kubwa ya utani wa vijana na wazee ni matumizi ya lugha, ambapo, utani wa vijana hutumia lugha kali na ya wazi wakati utani wa wazee hutumia tafsida kwa kiasi kikubwa. Anafafanua kuwa utani huo huweza kutolewa kwa kutumia semi, simulizi au nyimbo ambazo zote ni sehemu za matumizi ya lugha. Kazi hii pia ilitoa mwangaza katika utafiti wetu kutokana na kuhusiana kwa kiasi kikubwa.

Fenn na Perullo (2000) wamezungumzia kuhusu uchaguzi wa lugha unaofanywa na wanamuziki wa *Hip hop*. Wao wanasema kuwa hali ya sasa ya mabadiliko ya kiuchumi na kijamii imetoa mchango mkubwa katika maendeleo ya muziki wa Hip hop. Na kwamba, kuna uhuru wa kuchagua lugha katika *Hip hop* ya Tanzania iwe ya Kiswahili, Kiingereza au kwa kuchanganya lugha zote mbili. Hali hii inaakisi itikadi inayosimamiwa na mwanamuziki wa *Hip hop*. Wanatumia lugha ya Kiingereza kwa lengo la kupata hadhira pana. Kiingereza kinachukuliwa kama ni lugha ya kisiasa ya kimataifa na Kiswahili kama ni lugha ya taifa. Utafiti wetu unafanana kwa kiasi fulani na wa akina Fenn, kwani, sisi hatukuishia tu katika kuangalia uchaguzi wa lugha katika muziki wa kizazi kipya, bali pia, tulizama zaidi katika kuangalia matumizi ya lugha katika muziki wa kizazi kipya katika tungo zinazozungumzia suala ya mapenzi kwa wasanii teule.

Chachage (2002) anafafanua kuhusu utandawazi na migogoro ya kiutamaduni Tanzania. Anasema kuwa wanaodhani muziki *wa Hip hop* unaharibu utamaduni wa watanzania ni wapotofu wa mawazo, kwani, utamaduni wa jamii ni mwingiliano wa mambo mengi kutoka ndani na nje nchi husika. Anaona kuwa fasihi ya kiafrika na mtindo wake wa muziki vinaathiri *hip hop*. Anatoa mfano wa matumizi ya utani na misimu katika kuzungumzia masuala mbalimbali ya kijamii, kisiasa, kiitikadi na kiuchumi katika jamii. Utafiti wa Chachage nao unahusiana na utafiti wetu; kwani, yeye naye aliangalia matumizi ya lugha katika muziki huu ambao aliuita muziki wa *hip hop* kwa kuhusisha na utamaduni wa Kiafrika, wakati sisi, tulijikita zaidi katika kuangalia matumizi ya lugha ya muziki wa kizazi kipya husasani tungo za mapenzi za wasanii teule.

Senkoro (2003) katika makala yake ya "*Sanaa Pendwa na Utamaduni Afrika Mashariki Katika Karne ya Ishirini na Moja"* anasema wasanii wanatumia muziki wa Hip hop kama njia ya kuelezea msononeko, kukata tamaa na matarajio yao katika maisha ya kila siku. Vievile kazi ya Senkoro inahusiana na utafiti wetu licha ya sisi kujikita katika katika kufanya utafiti wa matumizi ya lugha ya muziki wa kizazi kipya yeye alijikita katika kuangalia maudhui ya muziki huu na matarajio ya wasanii wa muziki wa kizazi kipya.

Ponera (2010) akimnukuu Chuachua (2008) ambaye anazungumzia matumizi ya taswira katika riwaya za Shaaban Robert, anafafanua aina mbalimbali za taswira, mbinu zilizotumika kuziunda, pamoja na athari yake kwa hadhira. Kazi hii pia ilitoa mchango mkubwa katika utafiti hasa katika suala la matumizi ya Taswira. Hii ni kwa sababu matumizi ya lugha ndio kiini cha utafiti wetu. Aghalabu, huhusisha suala la matumizi ya lugha ya picha ambayo ni kiini cha kujenga taswira. Hata hivyo, utafiti huu ulikuwa kama kichokoo kwetu kutokana mbinyo wa mawanda ya malengo yake.

Mangesho (2003) alifanya utafiti wa muziki wa Hip hop uliokuwa wa Kisosholojia. Utafiti huo ulikuwa na lengo la kuchunguza mambo yaliyochangia muziki wa bongo fleva kusambaa na kupata umaarufu miongoni mwa wakazi wa Dar es Salaam. Utafiti ulionesha kuwa mambo yaliyochangia hilo ni kama vile kurekodi kwa kutumia kompyuta, na kuanzishwa kwa vituo vya redio vya Fm ambavyo vilikuwa chanzo cha kurusha nyimbo hizo. Mifano ya vituo hivyo ni *Radio One*, *Clouds Fm, Times Fm, Uhuru Fm* na kadhalika. Jambo jingine ni Kuanzishwa na kusambaa kwa kampuni za kurekodi muziki kama vile *Wananchi Stores, Bongo Records* na nyinginezo. Utafiti wa Mangesho unahusiana na utafiti wetu kwani umetusaidia

kutupatia historia ya muziki wa *Hip hop* Tanzania licha ya kuwa utafiti wake ulijikita zaidi katika masuala ya kisosholojia.

Perullo (2003) alifanya utafiti juu ya aina ya miziki maarufu inayopatikana katika miji ya Tanzania ambayo ni *taarab*, *Hip hop*, *Raggae*, *mchiriku* na *ngoma*. Alifanikiwa kufanya mahojiano na watu mbalimbali ambao wanaojihusisha na muziki kwa namna mbalimbali kama vile *Ma-DJ's,* wanamuziki, watayarishaji wa muziki *(producers*), wasambazaji *(Distributors*) na waandishi wa habari kutoka kwenye vyombo mbalimbali vya habari. Alikuwa na lengo la kutaka kujua njia wanazotumia katika kurekodi, kuzalisha, kusambaza, kuuza na kucheza muziki. Aligundua kuwa kuna njia mbalimbali zinazotumiwa na watu hao ili kukabiliana na mazingira ya kijamii, kiuchumi na kisiasa Tanzania kati ya njia hizo rushwa, uchawi, wizi na ushirikina kati yao na ndugu jamaa na marafiki huchukua nafasi kubwa.

Mwamzandi (2001) naye aliwahi kuandika kuhusiana na muziki, yumkini yeye alijikita zaidi katika kuangalia muziki wa taarabu hususani taarab ya mipasho. Aliona taarabu ya mipasho kwa hivi sasa ni muziki ambao nyimbo zake nyingi hujikita katika kufafanua zaidi masuala ya mapenzi. Mapenzi ambayo hivi sasa hunadiwa hadharani bila ya kificho wala soni. Watoto na vijana wengi wanaonekana kuvutiwa mno na nyimbo za mipasho, na hivyo, kuwafanya waingie kenye suala la mapenzi na mahusiano wakiwa katika umri mdogo. Andiko hili la Mwanazandi, licha ya kuwa limeangalia suala la matumizi ya lugha katika mipasho kwetu, limetusaidia kutoa ithibati angavu kuhusu kuwapo kwa utangamano wa dhahiri juu ya aina hizi za muziki wa kizazi kipya ikiwemo mipasho kama sehemu ya muziki wa kizazi kipya kwa kiasi kwa upande wa taarabu.

Mzee (2011) anafafanua athari wazipatazo wanajamii kutokana na matumizi ya lugha inayotumika katika muziki wa taarabu. Pia, anaelezea namna ya uchezaji (minenguo) ya muziki wa taarab unavyochangia  kupoteza asili yake na kuwa wa kisasa zaidi na hata kuharibu maadili ya wanajamii, hususani, jamii ya wazanzibar ambako utafiti wake alipoufanyia. Utafiti huu pia umekuwa chachu kwetu ya kutaka kufanya utafiti kuhusiana na matumizi ya lugha katika muziki wa bongo kizazi kipya na ulikuwa kama kichokoo kwetu yumkini kwa lengo la kuunda kazi yetu.

Mandalu (2008) alifanya utafiti juu ya matatizo yanayowakumba wanamuziki wa bongo fleva katika harakati zao za kujikwamua kutoka katika tatizo la ukosefu wa ajira. Anauona muziki wa *hip hop* kama ni chanzo cha ajira halali kinachowasaidia vijana wa Tanzania kujikwamua kutoka katika tatizo hili la ukosefu wa ajira nchini Tanzania na ulimwenguni kote kwa ujumla. Utafiti wa Mandalu unahusiana na kazi yetu kwa namna fulani. Licha ya yeye kujihusisha moja kwa moja na matatizo yanayowakumbuka wanamuziki wanaoimba muziki aliouita bongo fleva, sisi tumejihusisha na matumizi ya lugha katika muziki huohuo ambao sisi tumeutambulisha kama muziki wa kizazi kipya hususani katika tungo zinazohusu mapenzi kwa wasanii teule.

Omari (2009: 162-168) anajadili kuhusiana na matumizi ya misimu katika muziki wa hip hop huku yeye akiuita muziki wa bongo fleva. Anasema kuwa moja kati ya sifa zinazotofautisha muziki wa bongo fleva na aina nyingine ya muziki wa Kitanzania ni matumizi ya misimu. Anasema kwamba misimu ni lugha ya mficho inayozungumzwa na kundi fulani la watu katika jamii, kundi lenye watu wenye utamaduni unaofanana wenye lengo la kuwatenga au kuwafanya watu wengine wasielewe wanachotaka kukieleza. Misimu hubadilika kulingana na wakati. Kwa

hiyo, kundi fulani la watu kwa wakati fulani wanazalisha aina fulani ya misimu yao. Omari anaigawa misimu hiyo katika makundi sita, ambayo ni misimu inayohusu ulevi, misimu inayowahusu wanawake na sehemu za mwili, misimu ya mapenzi, misimu ya mavazi, misimu inyohusu fedha, pamoja na misimu inayohusu UKIMWI na mipira ya kiume na kike ya kujikinga na magonjwa ya zinaa na UKIMWI. Utafiti wa Omari unahusiana na utafiti wetu licha ya yeye kujikita katika kuchunguza matumizi ya misimu lakini utafiti huu umetupatia mchango mkubwa katika kuielewa hip hop ya Tanzania ambayo ameiita kama bongo fleva, kupitia kazi hiyo tulipata mwanzo mzuri wa kuelewa lugha iliyotumika katika muziki huu *wa hip hop* na sababu za kutumia lugha kwa kuzingatia maudhui ya nyimbo na rika lililokusudiwa na msanii husika.

Omari (2009;162 -168) anaendelea kujadili sifa zinazotofautisha muziki wa hip hop na aina nyingine ya muziki wa kitanzania ni matumizi ya misimu. Anasema kuwa misimu ni lugha ya mficho inayozungumzwa na kundi fulani la watu katika jamii. Kundi lenye watu wenye utamaduni fulani unafanana wenye lengo la kuwatenga na kuwafanya watu wasielewe wanachotaka kukieleza. Misimu hubadilika ulingana na wakati hivyo kundi fulani la watu kwa wakati fulani wanazalisha aina ya misimu ambayo itatumiwa na kundi fulani la watu.Kazi ya Omari nayo ilikuwa ni kichokoo kwetu kuweza kupata mwangaza wa utafiti wetu huku tukihusisha na kazi hiyo ambayo kwa kiasi fulani ilizungumzia misimu kama sehemu ya utafiti wetu. Omari (2011:69-86) alijadili matumizi ya lakabu zinazotumiwa na wanamuziki katika muziki wa bongo fleva nchini Tanzania na namna lakabu hizo zinavyowatambulisha katika jamii. Makala haya kwa kiasi kikubwa yametusaidia sisi kama watafiti kuweza kujua sababu  zinazowanya wanamuziki wengi wa kizazi kipya kutumia lakabu kama sehemu ya majina yao. Ambapo sababu za kufanya hivyo ikiwemo na

kujitambulisha au utambulisho wa msanii kwa jamii, ukaribu wao kwa mshabiki wao muziki wa kizazi kipya, kujikweza na kuleta ushindani baina yao ili kuweza kuinua soko la muziki na muziki kwa ujumla mathalani Khalid Mohamedi kujiita TID (*Top in Dar*) kama ni namna ya kujikweza dhidi ya wasanii wenzake, Joseph Haule (*Profesa Jay*) na Khamis Mwijuma (*Mwanafalsafa* au *Mwana FA*) hawa waliamua kutumia lakabu hizo kama sehemu ya utambulisho wao kwa jamii kama wao ni wasanii wasomi kwa kujipa lakabu za vyeo vya wasomi na wanazuoni.

Nyamahanga (2012) naye anazungumzia matumizi ya lugha, yumkini yeye aliegemeza zaidi katika kuangalia nyimbo za kihehe nchini Tanzania. Katika tasnifu hiyo anaangalia namna lugha ya kihehe inavyotumika katika nyimbo za aina mbalimbali kama vile mbolezi, tumbuizi, chapuzo na ina nyinginezo. Utafiti wa Nyamahanga unahusiana na utafiti wetu kwa namna fulani kwani ulitusaidia kuweza kujua matumizi ya lugha yanavyotumika katika aina tofauti za nyimbo ambazo hutumika kuunda muziki wa aina mbalimbali.

Sanga (2011) anazungumzia taswira ya mwanamke katika mashairi ya wasanii wa kike wa muziki wa kizazi kipya Tanzania. Anabainisha changamoto wanazokumbana nazo katika kumsawiri mwanamke katika tungo zao, michakato wanayoipitia katika kutunga nyimbo zenye usawiri wa mwanamke na mwisho aliangalia ni kwa jinsi gani wasanii hawa wa kike wameweza kukwepa mtazamo hasi wa kumwangalia mwanamke licha ya kuwa wao ni wanawake. Utafiti huu wa Sanga unahusiana na utafiti wetu hususani, kwani, umetusaidia kwa kiasi kikubwa kuweza kujua asili ya muziki huu wa kizazi kipya ni kwa jinsi gani muziki huu pia ulivyoweza kuhusisha jinsia zote mbili katika utunzi na kwa jinsi muziki ulivyochangia kutoa ajira kwa vijana wa Kitanzania bila ya kujali jinsia.

Almasi (2012) anafafanua jinsi muziki huu ulivyotoa mchango mkubwa katika kukuza lugha ya Kiswahili nchini Tanzania. Utafiti huu ulitusaidia kufahamu chimbuko na historia ya muziki wa kizazi kipya na kuwafahamu waasisi na waanzilishi wa muziki huu nchini Tanzania, muziki wa hapo awali ulikuwaje na ni kwa jinsi gani unavyotofautiana na muziki wa sasa wa bongo fleva kifani na maudhui kama unavyosawiriwa na wasanii mbalimbali nchini Tanzania.

### 2.3 Mapengo Yanayopaswa Kuzibwa

Ingawa wataalamu mbalimbali wameshughulisha na kufanya utafiti katika kipengele cha matumizi ya lugha katika kazi za fasihi kama vile muziki, hususani, muziki huu wa kizazi kipya, tumegundua kuna mapengo yafuatayo: Kwanza, wengi wa wataalamu hao wameshughulikia kipengele cha matumizi ya lugha katika muziki wa kizazi kipya kwa ujumla wake na sio tungo zinazozungumzia mapenzi kwa upekee wake. Pili, uchunguzi wa wataalamu wengi umejiegemeza katika kubaini matumizi ya lugha kwa vipengele kama mitindo ya lugha, misimu na si katika sababu za kutumia lugha hiyo na wasanii pamoja na athari tungo za mapenzi kwa hadhira kupitia wasanii teule ambao tumewatafiti.

# SURA YA TATU

# USANIFU NA MBINU ZA UTAFITI

## 3.1Utangulizi

Sehemu hii inafafanua mpango wa jumla wa utafiti, eneo la utafiti, jamii za watafitiwa zana na mbinu za kukusanyia data, uhalali na uthabiti wa matokeo wa matokeo ya utafiti, mchakato wa kukusanya data pamoja na uchambuzi wa data.

## 3.2 Mpango wa Utafiti

Utafiti huu ulifanyika maktabani na uwandani. Mwelekeo wa utafiti huu ni wa kifafanuzi, hivyo haukujihusisha kabisa na taarifa za kitakwimu. Aina hii ya utafiti wa kiufafanuzi aghalabu hutumia mbinu za maelezo, ulinganisho, pamoja na uhusishaji wa data dhidi ya nadharia katika kuchanganua data zake na kutolea matokeo. Hivyo, ukusanyaji, uchanganuzi wa data, pamoja na utoaji wa matokeo ya utafiti huu uliegemezwa katika mbinu hii. Sehemu kubwa ya data za utafiti huu zilitarajiwa kuwa ni za kimaktaba kwa kuzihusisha na taarifa za uwandani.

## 3.3 Eneo la Utafiti

Utafiti huu ambao kwa kiasi kikubwa ni wa kimaktaba ulifanyika katika miji ya Dar es Salaam na Dodoma (Tanzania). Sababu za kuuchagua miji hiyo ni kuwa wanamuziki hawa teule wote wanapatikana katika jiji la Dar es Salaam. Pia kuteuliwa kwa miji hii mikubwa nchini Tanzania ni kutokana pia na kuwapo kwa vyuo vikuu vyenye maktaba na makavazi yaliyolengwa kutumiwa kwa ajili ya udurusu. Vyuo vikuu ambavyo vilitumiwa katika kutupatia taarifa za kimaktaba ni kama vile Chuo Kikuu cha Dodoma na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

### 3.4 Walengwa wa Utafiti

Walengwa wa utafiti huu wamegawanyika katika makundi mawili ambayo ni wango tafitiwa katika ujumla wake na sampuli itakayoshughulikiwa.

#### 3.4.1 Wango Tafitiwa

Taarifa za utafiti huu zinatarajiwa kupatikana kutoka katika makundi yafuatayo:

a) Nyimbo mbalimbali zinazozungumzia mapenzi na mahusiano za wanamuziki Inspekta Haroun na Mwanafalsafa. Hizi zilisaidia kubainisha matumizi ya lugha ya tungo hizo ambazo zimechambuliwa na watafiti.

b) Wanamuziki wa kizazi kipya ambao nyimbo zao zilitumiwa katika utafiti wetu. Hawa walitarajiwa kutoa taarifa za matumizi ya lugha katika tungo za mapenzi na namna zinavyoweza kuibua misimu mbalimbali.

c) Wananchi wa marika na jinsia tofauti wa jiji la Dar es Salaam (ambako kwa kiasi kikubwa muziki huu ndio unasikilizwa sana na wanamuziki hawa ndipo wanapoishi). Hawa walitarajiwa kutoa taarifa za matumizi ya lugha katika tungo za mapenzi za wasanii teule.

#### 3.4.2 Sampuli ya Watafitiwa

Sampuli ilipatikana kwa kutumia mbinu ya sampuli lengwa. Hii ni mbinu ya usampulishaji ambayo humruhusu mtafiti kuwachagua wawakilishi wa kutafitiwa kulingana kwa jinsi walivyokidhi haja na malengo ya utafiti huu. Mbinu hii hukidhi haja ya tafiti za kitaamuli kama hii ambazo aghalabu hujihusishaa zaidi na kutoa ufafanuzi na maelezo kuliko takwimu. Sampuli yenyewe ilijumuisha yafuatayo:-

a) Nyimbo nne kwa kila mwanamuziki teule wa utafiti huu. Kwa upande wa Inspekta Haroun, nyimbo zilizotumika ni “Asali wa Moyo”, “Asali wa Moyo (remix)”, “Mtoto wa Geti Kali”, na “Bint Kisura”. Nyimbo za Mwanafalsafa zilizochambuliwa ni “Hawajui Tulikotoka”, “Unanitega”, “Wanazimika” na “Alikufa kwa Ngoma”.

b) Wataalamu kutoka taasisi za BAKITA/TATAKI na wataalamu wa muziki kumi, ambao wamewahi kufanya shughuli za muziki hapo awali kwa namna fulani kama vile wanamuziki wa zamani, watu wenye taaluma ya muziki kwa kusomea pamoja na watayarishaji wa muziki wa kizazi kipya.

c) Watu wazima wenye umri kuanza miaka arobaini na kuendelea wanawake na wanaume ishirini (20), ambao wanaishi katika miji ya Dar es Salaam na Dodoma ambao wanaufahamu na kuufatilia muziki wa kizazi kipya kwa kuusikiliza na kuuchambua muziki huu. Lengo la kutumia rika hili ni kuweza kupata mtazamo wao juu ya matumizi ya lugha ya muziki wa kizazi kipya na kujua namna unavyopokelewa na kundi hili.

d) Vijana ishirini (20) wenye umri wa kuanzia miaka kumi na minne mpaka thelathini na tano (14-35) wa jinsia zote ambao wanapatikana katika miji ya Dar es Salaam na Dodoma ambao ni wasikilizaji na wafuatiliaji wazuri wa muziki wa kizazi kipya. Lengo ni kujua mtazamo wao na maoni yao kuhusiana na matumizi ya lugha ya muziki wa kizazi kipya na hata kujua namna wanavyoupokea muziki wa kizazi kipya.

### 3.5 Ukusanyaji wa Data

Sehemu hii inaelezea njia na zana mbalimbali zilizotumika katika kukusanyia data pamoja na mchakato wa kukusanya data.

### 3.5.1 Njia na Zana za Ukusanyaji wa Data

Njia kuu zilizotumika katika kukusanya data za utafiti huu ni udurusu wa kimaktaba, ushuhudiaji na mjadala wa vikundi, vijidaftari, kalamu, kamera ya picha za mgando na kinasa sauti.

#### 3.5.1.1Udurusu wa Kimaktaba

Ni utaratibu ambao unahusisha kwenda maktabani kudurusu na kupitia maandiko yanayohusiana na mada ya utafiti. Miongoni mwa maandiko yaliyopatikana maktabani kwa ajili ya udurusu ni kama vile tasnifu mbalimbali zinazohusu matumizi ya lugha na muziki wa kizazi kipya, majarida pamoja na vitabu vinavyohusiana na mada ya utafiti. Hapa matumizi ya madaftari yalitumika kama zana ya kukusanyia data na kuhifadhi taarifa ambazo zitapatikana katika maktaba zilizotembelewa na mtafiti kwa kipindi chote cha utafiti huu.

#### 3.5.1.2 Ushuhudiaji, Mjadala wa Vikundi na Usaili

Ni utaratibu ambao ulimhusisha mtafiti na timu yake kwenda uwandani kukusanya data. Njia zilizotumika ni pamoja na kushuhudia matumizi ya lugha yanavyotumika kusawiri vionjo vya mapenzi katika nyimbo za wasanii teule kwa jamii, sababu zilizowasukuma wasanii kutunga nyimbo hizo na athari wazipatazo jamii kutokana na nyimbo hizo. Majadiliano ya vikundi pamoja na usaili kwa wasanii teule kuhusiana na kujadili malengo mahususi ya utafiti huu ambapo zana kama vijidaftari, kalamu, kamera na vinasa sauti vilitumika katika kukusanya na kuhifadhi taarifa zilizopatikana uwandani.

### 3.5.2 Mchakato wa Ukusanyaji wa Data na Udhibiti Wake

Utafiti huu ulizingatia maadili yaongozayo mchakato wa utafiti. Kwa mujibu wa Ponera(2014), maadili hayo hujengwa na masuala kama vile uombaji wa ridhaa ya watafitiwa, utunzaji wa siri za taarifa na ufichwaji wa majina ya watoa taarifa kadiri ya matakwa ya watafitiwa. Yote haya yalizingatiwa. Data za maktabani zilikusanywa kwa njia ya udurusu, ambapo mwongozo wa udurusu ulitumiwa. Hivyo mwongozo huo ulitumika katika kusoma tasnifu, vitabu majarida na vielelezo mbalimbali vihusianavyo na utafiti huu.

Data za uwandani zilikusanywa kwa njia tatu ambazo ni ushuhudiaji, mjadala wa vikundi pamoja na usaili ambao ulitumika katika kuwasaili wasanii teule wa muziki wa kizazi kipya ambao tungo zao za mapenzi zilitumika katika utafiti huu, wasanii hawa wote wawili walipatikana mkoani Dar es salaam,Tanzania. Kwa mujibu wa Kothari (2009), "Usaili kama njia ya ukusanyaji wa data hurahisisha upatikanaji wa taarifa za kina kutokana na kumruhusu mtafiti kusaili vipengele vya nyongeza". Mwongozo wa ushuhudiaji ulitumiwa wakati wa kushuhudia utendekaji wa tungo za mapenzi katika jamii ambazo msanii amewatungia na kuwaimbia tungo hizo. Mjadala wa vikundi ulitumiwa na kundi teule la watu ambao limeshabainishwa hapo awali. Mtafiti aliongoza mjadala kuhusu dhana ya mapenzi kama ilivyotumiwa na wasanii hawa katika tungo zao. Vinakilishi kama vile daftari na kalamu vilitumika katika kunukuu na kuandika taarifa zilizopatikana katika mahojiano na udurusu kwa ajili ya kutumika wakati wa uchambuzi wa data. Vifaa vingine kama vile kamera na kinasa sauti vilitumika katika kuwarekodi wasawiliwa na kupiga picha na vielelezo mbalimbali vihusianavyo na utafiti huu.

### 3.6 Uchanganuzi wa Data

Uchanganuzi wa data za utafiti huu ulifanywa kwa kutumia mihimili ya nadharia ya Umuundo. Data zilichanganuliwa kwa kuzingatia malengo ambayo yamebainishwa hapo awali kuhusu utafiti huu. Data zilizopatikana uwandani kupitia njia za usaili na majadiliano ya vikundi zilichanganywa na kuwianishwa na na zile zilizopatikana kutokana na udurusu wa kimaktaba kisha kupimwa na kutathminiwa. Baada ya uchanganuzi huo, matokeo yametolewa kwa njia ya maelezo ambayo yalitumika kwa kiasi kikubwa.

### 3.7 Uhalali na Uthabiti wa Matokeo ya Utafiti

Ponera (2014) anafafanua kuwa uhalali wa utafiti ni ile hali ya utafiti kuwa na uwezo wa kupima jambo au mambo yaliyotakiwa kupimwa au kutafitiwa tu. Na uthabiti wa utafiti ni ile hali ya utafiti kuweza kutoa matokeo yanayoendana ikiwa utafiti utafanyika wakati mwingine, mahali pengine au hata na kufanywa na mtu mwingine kwa mada ileile. Vipengele hivi viwili vina uhusiano wa kimjalizo. Anaendelea kusema kuwa ni vigumu kwa utafiti kuwa na matokeo thabiti ikiwa uhalali utakosekana.Kwa hiyo, aghalabu, uhalali wa matokeo ya utafiti huu hutarajiwa kuthibitishwa kwa kutumia mbinu zifuatazo: Mosi, kwa kuweka bayana malengo na mipaka ya utafiti. Pili kwa kutumia lugha nyepesi na ya moja kwa moja katika zana za kukusanyia data ili sampuli isipate tabu ya kuelewa kinachotafitiwa na hivyo, kutoa majibu yatakayohusiana na malengo ua utafiti huu. Tatu kwa kutumia njia za ukusanyaji data kama vile usaili, ushuhudiaji, udurusu, pamoja na mjadala wa vikundi lengwa. Kwa kutumia mbinu hizi matokeo pia yalikuwa na kiwango kikubwa cha uthabiti. Hivyo basi, mtafiti alijiegemeza katika mawazo hayo ya Ponera katika kujenga uhalali na uthabiti wa matokeo ya utafiti uiofanyika.

### 3.8 Changamoto za Utafiti na Utatuzi Wake

Katika kipindi cha utafiti hususani wakati wa ukusanyaji wa data, mtafiti alikumbana na changamoto mbalimbali kama vile; Changamoto kubwa ilikuwa ni kitendo cha watafitiwa kudai fedha ili waweze kuhojiwa na mtafiti na wakati mwingine ilijitokeza hali ya kudai malipo baada ya mahojiano na mtafiti. Hii ilitokana na kuamini mtafiti anapata faida kubwa za kiuchumi kutokana na matokeo ya utafiti huo, huku watafitiwa kutopewa fedha wala kuambulia chochote zaidi ya asante ya mikono mitupu. Utatuzi wa changamoto hii ilikuwa ni kutoa elimu kuhusu manufaa ya utafiti huu kwa jamii ya wanataaluma na jamii kwa ujumla.

### 3.9 Mipaka ya Utafiti

Utafiti huu ulichunguza jinsi matumizi ya lugha yanavyojitokeza katika tungo za mapenzi katika muziki wa kizazi kipya, hususani, zile za wasanii Mwanafalsafa na Inspekta Haroun. Kazi zao ambazo hazizungumzii mapenzi hazikuzamiwa. Baadhi yazo zilizamiwa kwa jicho la jumla katika kutafuta muwala au ithibati zaidi kuhusu matumizi ya lugha yanavyoweza kuibua misimu mbalimbali ya lugha ambayo hutumika katika Kiswahili.

# SURA YA NNE

# MJADALA WA MATOKEO YA UTAFITI

## 4.1 Utangulizi

Sura hii imegawanyika katika sehemu nne ambazo ni matumizi ya lugha zenye vionjo vya mapenzi katika muziki wa kizazi kipya, sababu za kutumia tungo za namna hiyo, athari zavionjo vya kimapenzi katika nyimbo za wasanii teule na mwisho ni muhtasari wa sura.

## 4.2 Matumizi Ya Lugha Zenye Vionjo Vya Mapenzi Katika Muziki Wa Kizazi Kipya

### 4.2.1 Muhtasari wa Nyimbo Teule za Inspekta Haroun

Nyimbo teule za mapenzi za msanii Inspekta Haroun kimaudhui kwa kiasi kikubwa zinazungumzia mapenzi, hasa ya jinsia mbili tofauti. Yawezekana mapenzi hayo ni baina ya mume na mke au ya mtu na mchumba wake. Kimsingi, nyimbo za msanii huyu zimeegemea katika kumuelezea mwanamke kwa kutaja wasifu wake wa nje (muonekano) pamoja na wasifu wa ndani (kitabia). Kwa upande wa fani, kwa kiasi fulani msanii amekuwa akichanganya lugha kwa kiasi kikubwa katika tungo zake. Anatumia Kiswahili fasaha na lugha ya mtaani ambayo imesheheni misimu kadhaa. Nyimbo teule za msanii Inspekta Haroun kama zilivyobainishwa hapo awali ni kama vile, “Bint Kisura”, “Asali wa Moyo”, “Mtoto wa geti Kali” na “Asali wa Moyo (remix).

#### 4.2.1.1Wimbo wa “Mtoto wa Geti Kali”

Kiitikio; Nimekufia fia, nimekuzimikia kia, mtoto wa geti kali

kwa kuwa maisha yangu ya geto kukuambia naona hatari

kama unaweza *baby* njoo tujivinjari

lakini jeh! jeh! unanaweza kula ugali na kurumangia na kachumbari!

kachumbari

Nasimama mbele ya umati jamii na kadamnasi, nahisi kuvuja jasho jembamba na mtiririko wa kamasi

Siyo siri kwa mtandao huu Inspector nimeuwawa, kikatili kwa kumpenda mtoto wa *kikaladi*

*Bambadi* mweusi uso softi usio chunusi *natural* kala, chotara mrefu mng’avung’avu maji ya kunde

Kaenda hewani sekunde, kwao Obei Osterbay, Masaki binti huyu mtanashati mbwa mkali

Geti kali mambo safi, super sio diseli, usafiri wa kifahari *chesa* mayai vioo vya *batani*

Ndani ina viyoyozi, kila siku akitaka gari *anachenji, korando rozi-rozi range mara melsidis benzi*

Wakati msela kabwela, kajamba nani, maisha Uswahilini, Temeke Mikoroshini sina hata baiskeli

Domo gundi limejaa mate, ute halafu nashindwa kumweleza ukweli stori mi na huyo shori zinapanda kichizi sometime demu ananiuliza - Inspector “sema basi unataka nini” mi nabaki mmh! Mmh! a e i o

Nabaki na kigugumizi, nikimcheki wakati kaweka *pozi* ohoo!ohoo! ee bwana wee!,nicheki *sister* haswa, alieumbika haswaa, amepambika haswaa, *makosmetics enjoface* na mavimbwaga *yose* na vipodozi lakini

*Kumtel live* inakuwa *imposible*, mi naona gozi gozi, nimemfia fia nimemzimikia kia mtoto wa geti kali

*Hips figa figali*, mstari, domo gundi, kumwambia naona hatari cheki mtoto alivyo jaza, jazia kafunga funga shia guu la bia, mmh! Mmh! *iwe bojo* sijui nimwambie, sijui nikae chini nilie,

Napata kigagaziko, domo lina ujauzito utafikiri haendi chooni

Isitoshe likizo zake ni *South Afrika*, Amerika au mamtoni

Tatizo ni pale atakakapohitaji kutembela nyumbani

Wakati kwetu jumba la udongo choo cha makuti *paspoti size*

Nitonye nitamkaribisha wapi kwao keshazoea kuketi sofani,

*Siting room varandani* jicho kideoni msosi wa *draft self service*

mboga saba *kujisevi*a kwetu ngangari dona bamia aah  ananipagawisha

Kiitikio

Nimekufia fia nimekuzimikia kia mtoto wa geti kali

kwa kuwa maisha yangu ya geto kukuambia naona hatari

kama unaweza *baby* njoo tujivinjari

lakini jeh!jeh! unanaweza kula ugali na kurumagia na kachumbari!  kachumbari

Mtoto wa geti *mankret* pamba zake *vibodi taiti*

Ana mandhari ya *kimiss* nywele mithili ya Jenifa Lopez

*Figa na swing slide* zake mtaani kote hadithi

Mdomo umekolea *shedo lipustiki* wa kunyonya denda

*baiti love roman*ce ngozi nyororo mororo murua

mwili utafikiri kamwagiwa asali ana pua

ndefu ndefu ya kikabachori kila nikimchunguza sioni hata dosari

ama kweli kupenda ni ugonjwa wa donda ndugu

sijui niseme nini huyu kimwana jinsi nilivyomhusudu

mtoto ziwa chuchu saa sita kajazia haja kubwa mgongo bambataa

taarabu anayao ukicheki nyoro inapwita

Chu! Chu! Chu! To! To! Toooo! Ajigijigijiii

Aah jamani nashindwa, hata hela ya kumnunulia bigijii

Isitoshe huyo mchumba, kwao wana mavumba

Goto limekata mapene yamecheua mtoto wa geti kali

kidosi dosi tena kishua elimu imepanda kenda kidato kabukua

Anatema *slang*, anamwaga ngeli, anabonga ung'eng'e *Kilatin Spanish*

*French* hapo ndo chenye mambo *leshen* msosi

ma kila kitu kwao *stoku bifu kao* kitimoto *pork*

Ndani ya *frige friza* vimiminika vya kumwaga lilu mpaka kusaza weeh!

***Kiitikio***

*Nimekufia fia nimekuzimikia kia mtoto wa geti kali*

*kwa kuwa maisha yangu ya geto kukuambia naona hatari*

*kama unaweza baby njoo tujivinjari*

*lakini jeh! jeh! unanaweza kula ugali na kurumangia na kachumbari! kachumbari*

Huu ni wimbo wa mwanzoni kabisa wa msanii huyu ambapo aliurekodi akiwa na kundi lao la Gangwe Mob kwa kushirikiana na msanii mwenzake Luteni Karama[6].

[6] Luteni Karama – ni miongoni mwa mwaanzilishi mwenza wa kundi la muziki wa hip hop la Gangwe Mobb lenye maskani yake Temeke Mikoroshini, Dar es Salaam. Kundi hili waliwahi kutamba na nyimbo kali kama vile "Mtoto wa Geti Kali", "Nje Ndani", "Mzee wa Busara".

Huu wimbo uliomtambulisha msanii Inspekta Haroun na kundi zima la Gangwe Mob katika medani ya muziki wa kizazi kipya katika miaka ya 1998 – 2000. Maudhui ya wimbo huu nayo ni ya mapenzi. Ni mapenzi ambayo yanaelezewa na watu wa matabaka mawili tofauti. Mwanaume anatokea tabaka la chini kiuchumi wakati mwanamke yupo katika tabaka la juu. Hata hivyo, wanaamua kuweka mbali tofauti hizo na kuwa katika mahusiano

#### 4.2.1.2 Wimbo wa "Asali wa Moyo"

"Asali wa Moyo" – Inspekta Haroun

Hizi ni tunzi madhubuti kauli safi na kimahususi

Kwako mupenzi suala hili liko wazi tokea enzi enzi

Na sio siri tena na sibaki a e i o u hapana

Sina kigugumizi tena na domo sio gundi tena

Kinywa chepesi laini murua maridadi kabisa

Maneno natema uhuuu! Nashusha pumzi nahema

Mwana wa Kahena nimekufa kimahaba

Unanichanganya kwa mambo mengi sana

Kisura, kiumbo mshobo mpaka uroda

Najua wanakutazama kwa jicho la husda mama

Mtoto kichungwa *kipotabo* tena bomba

Ni wao tuu na roho zao za choyo

Wewe ndio asali wangu wa moyo

Sitojali wanite zoba nimerogwa ama poyoyo

Wanataka kuzua mkunungu na jakamoyo

Kutwa tuneno tudogo tudogo tusikupe shaka saana

Twende bega kwa bega kama samaki na maji

Mizizi na ardhi tuzidi kuwachanganya

Kiitikio – Wewe ndio asali wangu wa moyo

Kwa dhiki na faraja mpenzi kaza moyo

Ingawa yatasemwa mengi midomoni mwao

Usiwajali hao

Ewe ndio asali wa moyo wangu, wa nyuma yako wote nawaona machangu wa *town*

Nakupa shada uvumilivu, kwa wako utulivu, sogea soo tuzile zetu mbivu

*Honey! wao crazy, I can't believe* nilipoanza kukutokea, kukufukuzia

Wana walianza kupaka tena kukandia. Aah! Inspekta huwezi kung'oa mtoto *high classic*

Yaani mgumu kama kisiki, hang'oleki hata kwa leki

Nikijicheki hali yangu duni, halafu sina *uspuni town*

Kwetu chai rangi, vitumbua andazi, Nyumba mbavu za mbwa,

Aliye nje anatuona waziwazi, wakati shori kwao mambo ya mshiko

Midikodiko chai, ziwa, juisi, pesheni, embe, miwa

Rosti maini, tambi koronya, laini laini na vyapati vyapati

Aaah! ningempata wapi?Mmh*! Iwe bojo kaisi nikwenda munoo akanana kage,*

*Nikushaba ighonzi*. Wanga wameuwawa mtaani, mchuchu kujivinjari nami

kila tozi anayemtokea anamuona kama Osami

Uu unajua wengine hawajui maana ya kupenda

Uu unajua wengine wanaona uchafu hata kulamba denda

Uu unajua wengine wanahofu kukashifiwa kwa kuwatokea watoto wa matajiri

Au woga kupigwa kalenda. Waa wangejua mapenzi hayachagui fukara, mtawala, dini, kabila, desturi mila kama mi na bi Shada tumependana mradi

tumeshibana weh weh asali wa moyo

Kiitikio – Wewe ndio asali wangu wa moyo

Kwa dhiki na faraja mpenzi kaza moyo

Ingawa yatasemwa mengi midomoni mwao

Usiwajali hao

Kwa mujibu wa Inspekta Haroun alipokuwa akihojiwa na timu ya watafiti alisema kuwa wimbo huu aliutunga mnamo mwaka 2004 alipokuwa katika mahusiano ya uchumba na mkewe Sada Bint Salehe. Maudhui ya wimbo huu ni ya mapenzi, kwani amezungumzia namna anavyompenda mpenzi wake ambaye kwa sasa ni mke wake. Ametumia tamathali za semi kama sitiari kwa kumfananisha mpenzi wake huyo na asali. Asali ni kinywaji kinachoaminika ni kitamu zaidi ya sukari. Ameongezea kuwa asali wa moyo kama utamu/furaha ya moyo, anajivunia kuwa na mpenzi wake na anafurahi yeye kuwa chaguo pekee la mpenzi wake ambaye ameridhika kuishi naye kwa hali zote za maisha, mathalani starehe na shida.

#### 4.2.1.3 Wimbo wa "Bint Kisura"

Aaah! Aaah! Hii nyingine tena…! Agis sikia stori ya bint Kisura

Kiitikio; We bint Kisura nakupenda kuliko kula

Mimi nakutata twende tukajichane bata

Aaah! Aaah! Mimi naogopa kwanza tukapime ngomaa

Halafu naenda kusoma ndoa itafuata

Wala usiwe na pupa

Bint kutoka maziwa makuu, mwenye kipato cha nafuu

Kifua konzi sio mtindi chuchu, kifuu akiongea anabonga

Analonga kama ana mafua, kwa kizungu fluu – *Hellow*

Kafungashia *hips*, kajazia nyonga,  kaning'iniza cha bei mbaya

Kilonga longa ana simu ya ukali, ina *MP4 Bluetooth* na kamera

Hang'oki hata ukija na fuko la mihera, uzuri wake kama redio

Dabo deka figure iliyojengeka, mpole sio machegeka anadeka

Mwendo wa kujiachia, maringo halali yake sio kama anajisikia

Ni bint aliyeumbwa, akaumbika, mapambo anapambika, tabia iliyosadikika

Ana viwango vya TBS, hana skendo wala tetesi, mcheshi haendi lesi

Mtaani anawasumbua makinda, vibopa, mpaka washua wengi washamtokea

Kwa gia ya kumuongopea, walijinadi mie ndo tupatupa unachotaka ntakupa

Utaishi kitajiri sio kilofa usafiri wa kumwaga, misosi ya kubofya *full* kipupwe

*Full* pamba yaani ndani *full* sofa, mtihani mdogo wakware uliwaumbua

Alipowashauri kupima ngoma kabla ya tendo la ndoa

"Tukapime basi" wengi walikimbia na kushindwa kumuopoa

Walitoka baruti – Ebana hii ni soo!

Kiitikio – We bint Kisura nakupenda kuliko kula

Mimi nakutaka twende tukajichane bata

Aah aah mimi naogopa kwanza tukapime ngoma

Halafu naenda kusoma ndoa itafuata

Wala usiwe na pupa

Wengi wananitokea, nnapowaambia kupima wanapotea

Wanaogopa kupima ngoma na kujua afya. Hawataki kujua afya wanataka

Maisha yangu kunipotezea, Majibu ya virusi yatawashtua

Ni bint mrembo, mwenye busara na upendo, akicheka mashavu yanabonyea

Mwenye *lips* nyembamba, pua ya kihindi na macho ya kusinzia

Nyusi na *sigh* ndefu, shingo ya *kimiss* nywele ya kimanga, utadata anavyotembea

Anavaa vivazi vya kutia mshawasha, pedo vinjunga na pamba za kuchengua

Senti ndogo ndogo anazo hazimpigi chenga, anazo anazo za kulumbua

Watu kibao walishapeleka posa bila ya cheti cha kupima ngoma, akatosa

Mwenendo na tabia zake, utatamani uwe wake

Kinachowashinda wengi ni ule msimamo wake

Ukimuangalia kwa pupa unaweza kuhisi kahaba

Ukweli humjui mwanaume zaidi ya miaka kumi na saba

Ukiwa tayari kupima ngoma, mdudu, minyenyere

Utakuwa chaguo lake utakae ishi nae milele

Utaendelea kubonjoa *katress* na kuchana bata

Na mapenzi shatashata kwa bint kisura

Mrembo ambaye hana matata

Kiitikio – We bint Kisura nakupenda kuliko kula

Mimi nakutaka twende tukajichane bata

Aah aah mimi naogopa kwanza tukapime ngoma

Halafu naenda kusoma ndoa itafuata

Wala usiwe na pupa

Wimbo huu nao unahusiana na mapenzi. Kwa maelezo ya msanii mwenyewe wimbo huu aliutunga mnamo mwaka 2005. Licha ya kuwa maudhui ya wimbo unahusiana na mapenzi lakini ni wimbo ambao unahamasisha kwa kiasi kikubwa suala la kupima afya ili kuweza kujua kama mtu ameathirika na magonjwa ya zinaa hususani UKIMWI. Vilevile anawahimiza wanawake kujenga tabia ya kujiamini na kuwa na msimamo imara kuhusiana na suala zima la mahusiano na mapenzi. Kifani, wimbo huu ametumia lugha ya mjazo pamoja na lugha ya picha ambapo amempamba na

kumsifu mwanamke kuwa ana sifa madhubuti za kiumbo na kuweza kumshawishi mwanaume yeyote kuwa naye kimahusiano.

#### 4.2.1.4 Wimbo wa "Asali wa Moyo (remix)"

Kiitikio; Tumevuka mabonde na milima vikwazo vingi tumesimama wiwa

Walishazusha vingi vioja asli wangu wa moyo tupo pamoja

Tumevuka mabonde na milima vikwazo vingi tumesimama wima

Walishazusha vingi vioja asali wangu wa moyo tupo pamoja

Penzi letu lilikumbwa na vikwazo sana, wewe ulivumilia wala hatukuachana

Walikwambia kila siku nina badili, wasichana uliwapuuza hukujali yao sana

Hao wanoko hao walishazusha vingi vioja asali wangu wa moyo tupo pamoja

Na kwenu nshaleta mi barua majibu nkajibiwa nimekubaliwa

Nachongoja wewe na mimi tufunge ndoa, washakunaku walishashindwa kutia doa

Wengine walikuja kwako kujigamba, uliweka masikio yako pamba

Wengine wakadiriki hata kuniponda, eti unampenda Inspekta fukara!

Eti unampenda msanii uchwara!, eti unampenda Inspekta fukara!

Eti unampenda msanii uchwara!

Anaishi Mikoroshiniii!

Oyaaa! Oyaaa! Oyaaa! Ksiii! Ksiii!

We sista antii nini unababaika babaika na msanii

Wasanii bongo! Njoo ujivinjari na sisi watu wenye mafedha na mali

Ntakupa *good time* debe nini unaruka mvinyo unapata vilevile

Eeeh! Eeeh! Samahani kaka, pesa ni zako, mali ni zako

Dharau zako huko huko, Ninachohitaji ni mapenzi ya kweli

Na kama nimekuudhi *sorry* kwa heri

Ishia wewe shori gani kwa nshakuthamiminisha hulipi wala nini piga bunda

Tazama maneno ya wakosaji washatoswa wamekuwa wapakaji

Usiwajali eeh wacha waseme sio hatari

Tazama maneno ya wakosaji washatoswa wamekuwa wapakaji

Kiitikio - Tumevuka mabonde na milima vikwazo vingi tumesimama wima

Walishazusha vingi vioja asali wangu wa moyo tupo pamoja

Tumevuka mabonde na milima vikwazo vingi tumesimama wima

Walishazusha vingi vioja asali wangu wa moyo tupo pamoja

Ewe ndio asali wa moyo wangu, wa nyuma yako wote nawaona machangu wa *town*

Nakupa shada uvumilivu, kwa wako utulivu, sogea soo tuzile zetu mbivu

*Honey*! Waooo! *crazy, I can't believe* nilipoanza kukutokea, kukufukuzia

Wana walianza kupaka tena kukandia. Aah! Inspekta huwezi kung'oa mtoto high *classic*

Yaani mgumu kama kisiki, hang'oleki hata kwa reki

Nikijicheki hali yangu duni, halafu sina '*uspuni town'*

Kwetu chai rangi, vitumbua andazi, Nyumba mbavu za mbwa,

Aliye nje anatuona waziwazi, wakati shori kwao mambo ya mshiko

Midikodiko chai, ziwa, juisi, pesheni, embe, miwa

Rosti maini, tambi koronya, laini laini na vyapati vyapati

Aaah! ningempata wapi?Mmh*! Iwe bojo kaisi nikwenda munoo akanana kage,*

Nikushaba ighonzi. Wanga wameuwawa mtaani, mchuchu kujivinjari nami

kila tozi anayemtokea anamuona kama Osami

Uu unajua, wengine hawajui maana ya kupenda

Uu unajua wenginea wanaona uchafu hata kulamba denda

Uu unajua wengine wanahofu kukashifiwa kwa kuwatokea watoto wa matajiri

Au woga kupigwa kalenda. Waa wangejua mapenzi hayachagui fukara, mtawala, dini, kabila, desturi mila kama mi na bi Shada tumependana mradi
tumeshibana weh weh asali wa moyo

Kiitikio - Tumevuka mabonde na milima vikwazo vingi tumesimama wima
Walishazusha vingi vioja asli wangu wa moyo tupo pamoja
Tumevuka mabonde na milima vikwazo vingi tumesimama wima
Walishazusha vingi vioja asli wangu wa moyo tupo pamoja

Rudia Kiitikio

Tumevuka mabonde na milima vikwazo vingi tumesimama wima
Walishazusha vingi vioja asli wangu wa moyo tupo pamoja
Tumevuka mabonde na milima vikwazo vingi tumesimama wima
Walishazusha vingi vioja asali wangu wa moyo tupo pamoja

Wimbo huu ni muendelezo wa wimbo wa awali wa "Asali wa Moyo" wa mwanzo. Msanii aliutoa wimbo huu kwa lengo la kuendeleza kile alichokianzisha katika wimbo wa awali, kwani kwa kipindi alichoutoa wimbo huu maisha yake ya mahusiano alikuwa tayari amekwishafunga ndoa na Bi Sada. Maudhui ni yaleyale ya mapenzi, kifani katika wimbo huu msanii amepamba lugha kwa kuchanganya lugha ya Kiswahili fasaha na Kiswahili cha mtaani. Kitendo cha msanii huyu kutumia lugha ya mtaani kwa kiasi kikubwa katika tungo zake kinatokana na kuishi maisha ya watu wa kipato cha chini huko Temeke Mikoroshini katika wilaya ya Temeke, mkoa wa Dar es Salaam.

### 4.2.2 Muhtasari wa Nyimbo Teule za Mwanafalsafa

#### 4.2.2.1 Wimbo wa "Alikufa kwa Ngoma"

Hakuonekana na binti hakuwahi kuiasi dini

Mfuasi mzuri wa maadili, lakini alikufa kwa ngoma.

Aliwarudisha waliopotea, akawapa tiba mbadala na

Adui mkubwa wa zinaa, lakini alikufa kwa ngoma

Najaribu kumjengea picha, mshkaji aliye kalala ndani ya futi sita

Namkumbuka mtaani, alipokuwa anakatisha na mara kadhaa

Maskani na washkaji ungemkuta, usingedhani anangoma

Machoni alivyokuwa mwema, mzuri mtanashati

Anayewaza kabla ya kusema. IBILISI wa njia za mwili

Daima alimchezea mbali, tungi vicheche mineli

Hakuonekana kujali, tazama maisha yake

Hutaliona kosa lake, kama aliefunga kufuli

katikati ya nyeti zake, mkali wa ushauri nasaha

aliongea kuhusu mapenzi, huku akipinga zinaa

ungesema achague kipindi angechagua njia panda

nyumba aipendayo, angechagua ya Ibada

utepe mwekundu mpaka kenye nguo za ndani

nadhani mimi najali wewe je?

Kama alikufa kwa UKIMWI jiulize alijali nini?

Kiitikio; Hakuonekana na binti hakuwahi kuiasi dini

Mfuasi mzuri wa maadili lakini alikufa kwa ngoma.

Aliwarudisha waliopotea akawapa tiba mbadala na

Adui mkubwa wa zinaa lakini alikufa kwa ngoma

Mara nyingi alikuwa mpole, mara chache alizongea wote tulimgeuza shule

Nasaha za bure kama tupo *class* vile, akatuasa kuhusu kuhusiana

Akatuonya kutoaminiana, mtazamo wake na wa mama Terry

Daima ulifanana, hadithi ya maisha yake ilikuwa safi kama nabii

Hakuna alieamini kama, mwisho wa mshkaji utakuwa wa namna hii

Gawa sana kondom na kufunza kama Angaza

Vijarida vya UKIMWI, yeye ndo alikuwa msambaza

Ina maana alikuwa anatoa, bila zake kubakiza

Ama amewekewa ufunuo wa mola anaonyesha miujiza

Siku zinakata hatumuoni, nini kasoro afya yake haieleweki

Eti imeanzisha mgogoro, leo anadunda kesho mgonjwa

Na hatoliacha godoro, alifanya kwa siri hadharani hakuna shahidi

Labda alivumilia sana, mwisho ukwasi ukamzidi

Ama ilikuwa kama ajali, aliepigwa na radi hatujui hatuweza

Sema na bado tunashangaa vipi, vipimo vinasema mshkaji alikufa kwa ngoma

Kiitikio; Hakuonekana na binti hakuwahi kuiasi dini

Mfuasi mzuri wa maadili lakini alikufa kwa ngoma.

Aliwarudisha waliopotea akawapa tiba mbadala na

Adui mkubwa wa zinaa lakini alikufa kwa ngoma

Sijaribu kubadili, nyekundu kuwa njano

Huu ni mfano kwamba UKIMWI ni kwa wote wembamba na wacheza sumo

Wazinzi wema pia, wamo na hauji kwa kufuata kimo

Ungezani upo salama, kuzidi usalama wenyewe

Ungedhani UKIMWI utaogopa, utamwacha mshkaji mwenyewe

Sivyo haufanyi utakavyo wewe, unafanya utakavyo wenyewe

Hakuonekana na binti hakuwahi kuiasi, dini mfuasi mzuri wa maadili

Lakini alikufa kwa ngoma. Aliwarudisha waliopotea akawapa tiba mbadala na adui mkubwa wa zinaa

Amsha akili janga kanga gani ulibebee

Siwaambie msiususie, sisemi zipu mzifungue

Sisemi muache kuwa wema, ila ujinga usiendelee

Kwamba kila aliyekufa kwa ngoma, ukadhani ni kicheche

Tuamini bado ni wenzetu, msiache wagonjwa wajifiche.

Kitikio - Hakuonekana na binti hakuwahi kuiasi dini

Mfuasi mzuri wa maadili lakini alikufa kwa ngoma.

Aliwarudisha waliopotea akawapa tiba mbadala na

Adui mkubwa wa zinaa lakini alikufa kwa ngoma

Jina la wimbo huu“Alikufa kwa Ngoma” limeundwa kwa msimu wenye maana ya kuwa “Alikufa kwa UKIMWI”, wimbo huu ulitungwa na Mwanafalsafa na kuimbwa kwa ushirikiano wa msanii Mwanafalsafa na Judith Wambura (Lady Jay Dee) mnamo miaka ya 2000. Licha ya kuwa ni utungo wa kimapenzi, lakini una upekee wa kuwahamasisha watu, hususani vijana, kujenga tabia ya kupima na kujua afya zao. Vilevile, kimaudhui, wimbo huu ulikuwa ukiwahamasisha watu kuhusu kuaminiana katika suala la mapenzi na mahusiano. Ulikuwa pia unapinga tabia za vijana kuwamini wenza wao na kupima kwa macho bila ya kwenda hospitali. Ndani ya wimbo huu amemchora kijana ambaye alikuwa mbali na anasa za dunia kama vile ulevi nauasherati lakini cha kushangaza, mwishowe kijana huyo alikufa kwa maradhi

ya UKIMWI na kuicha jamii katika mshangao kuhusu ambavyo kijana huyo aliupata ugonjwa huo mpaka akaaga dunia.

#### 4.2.2.2 Wimbo wa "Wanazimika"

**"Wanazimika" Mwanafalsafa ft Duly Sykes**

Binamu, *Handsome, we got* Majani *right here*

Kiitikio; Sio ajabu, sio hatari jamani

Hali imebadilika sio kama zamani

Sio tu kwa marijali, hata mabinti hutamani

Hakuna anayesubiri hofu watu wapo wazi – 'Wanapendana'

*Handsome*

Napenda vitovu ila naogopa shanga labda bado mtoto

Au labda bado mshamba wote wanavaa vikuku ili kuleta picha ya ngono

Wee subiri ipigwa *ragga* uone wanavyokata mauno

Wanavyopiga mipasuo usiseme wanavutia wenzao

Au vitovu vinavyoachwa wazi hawalengi jinsia yao

Magauni kama vioo ma broo ndio kusudio nyie ndo honey wao

*Bling bling* napigiwa simu nauliza we ni nani

Anasema ye ni Mariam sasa unataka nini eti utonane *Royal Palm*

Hiyo itakua ngumu haina shobo sitaki demu

Eeh! Eei! Eeei! Zigizoo FA Duly Sykes Majani

Kiitikio; Sio ajabu, sio hatari jamani

Hali imebadilika sio kama zamani

Sio tu kwa marijali, hata mabinti hutamani

Hakuna anayesubiri hofu watu wapo wazi – 'Wanapendana'

Nenda klabu siku za mabint bure

Washkaji huwa kibao utadhani wameambiwa wasilale

Wote wanakwenda *gym ili body* zivutie warembo

Ukidhani una mbinu mabinti wana mitego

Usiamini kuwa hawataki nawaelewa kwa mikogo

Wanatamani kuaproach wanaogopa kuitwa mlupo

*Hey! Hey! Hey!  Oooh! Noo* napata wazimu

Kila siku kukicha nasumbuliwa kwenye simu

Kila nikipokea wanaongea mademu

Hakuna wanachotaka zaidi ya kutaka nami game

*Heey! Nooh*! Zig Zoo Mwana FA

Kiitikio; Sio ajabu, sio hatari jamani

Hali imebadilika sio kama zamani

Sio tu kwa marijali, hata mabinti hutamani

Hakuna anayesubiri hofu watu wapo wazi – 'Wanapendana'

Ona maajabu ya jana Jack na Alice Viduka walipigana

Eti sababu yangu mbele ya watu wanazozana

Bado nasisitiza karne hii wanapendana

Wamchizika, marijali wanapenda ila mabint wanazimika

Imeshageuka sio kutongoza tuu warembo pia hulea akikupendana umechoka

Unanielewa acha vicheche kadhaa vinavyokomalia watu

Vyenye mapenzi ya mikwanja yani majina na umaarufu

Ambavyo ukiwa chata tu vinaonesha udhaifu

Wapo wanaotongoza  na bado ni waaminifu

Kiitikio; Sio ajabu, sio hatari jamani

Hali imebadilika sio kama zamani

Sio tu kwa marijali, hata mabinti hutamani

Hakuna anayesubiri hofu watu wapo wazi – ‘Wanapendana’

Wimbo huu nao ulitungwa na msanii Mwanafalsafa lakini aliuimba kwa kushirikiana na msanii mwenzake Abdul Sykes (Duly Sykes). Maudhui ya wimbo huu pia ni ya mapenzi kwa kiasi kikubwa. Amezungumzia suala zima la mapenzi na mahusiano ya wanawake na wanaume katika jamii. Jina la wimbo “Wanazimika” nalo limejengwa kwa kutumia msimu wa lugha wenye maana ya “Wanapenda”. Humo ameelezea mabadiliko ya maadili ya Kiafrika katika kuelezea hisia za wanaopendana; kuwa, sio lazima kila siku mwanaume tuu ndio wawe waanzilishi wa kusema hisia zao kwa wanawake. Mathalani anaposema kuwa;

“…Imeshageuka tu si kutongoza tu wanawake nao pia

hulea akikupenda na umechoka…”

Kifani, msanii ameupamba wimbo huu kwa kuchanganya lugha kwa kiasi kikubwa kwani, ametumia Kiswahili fasaha na lugha za mitaani kwa kuitambulisha kama misimu ya lugha.

#### 4.2.2.3 Wimbo wa “Hawajui”

Kiitikio; Hawajui tulipotoka, watajuaje tunapokwenda

Ya kwao yanawashinda, ya kwetu hawatoweza

Hawajui tulipotoka, watajuaje tunapokwenda

Ya kwao yanawashinda, ya kwetu hawatoweza

Suruali zinanifunguka vicheche vikikatisha

Mshahara ukitoka sirudi mpaka umekwisha

Nikirudi nane usiku nalala na viatu

Chicha chakali sikumbuki hata ndoa yetu

Nikiwa na wewe moyoni Napata aibu

Ukisoma macho utajua nnavyokughiribu

Sikawii kuharibu, nakosa sana adabu

Nakushangaa mwanamke una moyo ajabu

Siwezi kukuacha laaziz mwenyewe siwezi ishi

Tuliumbwa tuishi wote mpenzi weewe uishi na mimi

Umefunzwa utotoni umefundwa unyagoni

Kulea mwanaume lakini sio kama mimi

Usiku uliopita nlikupa ngeu mdomoni

Asubuhi ulipoamka ukasema umeniota mimi

Una mapenzi hata shetani angeyaogopa

Sirudishi hata robo ya unavyonipa

Hata washkaji zangu wanakiri kuwa sikufai

Kama ni adabu unastahili uzikwe hai

Kiitikio; Hawajui tulipotoka, watajuaje tunapokwenda

Ya kwao yanawashinda, ya kwetu hawatoweza

Hawajui tulipotoka, watajuaje tunapokwenda

Ya kwao yanawashinda, ya kwetu hawatoweza

Amani bila silaha niache tu niende laaziz

Usione huruma bado siyawezi mapenzi

Mi kicheche huniwezi usiogope kuniacha mpenzi

Kukusea ni ubinadam hakukuvui thamaniyoo

Watoto wan je kibao wote wasio na malezi

Na matusi ya mama zao yote huja kwako mpenzi

Nini unanipendea mwanaume nna sifa mbaya

Rafiki zako wote wananita Malaya

Napenda uwe na mume lakini sio mimi

Sitaki tuachane nakuomba uniache mimi

Ustahili uchezewe sistahili kuwa na wewe

Umefanana na utulivu uwekwe ndani na uolewe

Waweza kuta firauni peponi taulo langu niendapo bafuni

Nauli yangu niwapo safarini, usiendee mbali na mimi

Wangu u malkia kwa vile cheo kingine chochote hakitakufaa

Naamini utanisikia kwa vile unanizimia

Hata upewe dunia hautakaa kunirudia

Kiitikio; Hawajui tulipotoka, watajuaje tunapokwenda

Ya kwao yanawashinda, ya kwetu hawatoweza

Hawajui tulipotoka, watajuaje tunapokwenda

Ya kwao yanawashinda, ya kwetu hawatoweza

Huu pia ni wimbo ambao aliutunga Mwanafalsafa lakini aliuimba kwa kushirikiana na msanii mwenzake Judith Wambura (Lady Jay Dee). Maudhui ya wimbo ni ya mapenzi. Wimbo huu umebeba dhamira ya mapenzi ya kweli. Mapenzi hayo yanaoneshwa na mwanamke mhusika wa kwenye wimbo kwa mumewe kiasi cha kusema watu hawajui walipotoka na penzi lao hilo. Tofauti na hali ilivyo kwa mwanamke, huku mwanaume mhusika wa wimbo huu amechorwa kama mlevi,

mzinzi na asiye mwaminifu katika ndoa, lakini mwanamke ni mwaminifu ambaye ameapa kuilinda na kuitetea ndoa yake isije ikavunjika. Kifani msanii ameupamba wimbo huu kwa lugha nyepesi na ya kueleweka kwa kila rika. Ametumia misimu ya lugha kama vile “vicheche”, “milupo” akimaanisha wanawake wasiokuwa na utulivu yaani wahuni/malaya.

#### 4.2.2.4 Wimbo wa “Unanitega”

**“Unanitega” – Mwanafalsafa ft Nurah**

Mwana FA na Nurah tutaelewana baba *styles*

Kiitikio; Unanitega? Aaah! Mbona miguu ipo wazi?

Unanipenda? Aaah! Hebu uko! Mbona kifua kipo wazi?

Unanitega? Aaah! Mbona miguu ipo wazi?

Unanipenda? Aaah! Hebu uko! Mbona kifua kipo wazi?

Yaah! Yaah! Yaah! Kila niendako upo

Kila unionapo ni vituko sasa sema

Kama unataka tuwe mana shetwan

Kama unataka tuwe kaka na dada

Maah! Kama nahis midomo yako ipo *wet*

Unatamani unikiss udhani mi ni mwepesi

Unaamini *ntakudiss come tell me nigga please*

*Easy* sie hatuendi kwa style hizii

Wanyamwezi japo tumezaliwa Tz

Usiwatangazie wenzako eti unanipenda

Njoo moja kwa moja binti acha kuremba

Sitakuona kicheche, kwanza uko bomba

Huonekani mapepe huwezi sombasomba

Nastukia unavyotembea na zaidi ukiniangalia

Ni wazi unanizimia, kata shauri na kuniambia

Mchana unaumia na usiku unalia

Ukija kwangu unanichunia vipi unategea

Usiponiambia ni nini unategemea

Kiitikio; Unanitega? Aaah! Mbona miguu ipo wazi?

Unanipenda? Aaah! Hebu uko! Mbona kifua kipo wazi?

Unanitega? Aaah! Mbona miguu ipo wazi?

Unanipenda? Aaah! Hebu uko! Mbona kifua kipo wazi?

Wee njoo *serious* mama, njoo sema

Usijistukie zaidi, njoo sema

Unajipa *presha* za bure misele kichele

Ka kitoto cha shule adabu za kale mbele

Hudhani unaweza pendwa na mimi

Au uoga unashindwa kusema una nini

Usiwatume machizi wangu, naitaka kwa masikio yangu

Hata ukisema hadharani, naahidi sikuoni changu

Dhumuni nikushushie wasi – wasi

Kigugumizi kujikwaa sasa basi

Usigombane na *sister* ukadhani *ma Boo*

Yote kusema unasita unajipa tabu

Ukiniona unang’ata *lips* Auuma! Na macho yanazimika unaumwaa!

Msichana niambie naheshimu hisia zako

Azima jamvi kabla hawajaomba wenzako

Kiitikio; Unanitega? Aaah! Mbona miguu ipo wazi?

Unanipenda? Aaah! Hebu uko! Mbona kifua kipo wazi?

Unanitega? Aaah! Mbona miguu ipo wazi?

Unanipenda? Aaah! Hebu uko! Mbona kifua kipo wazi?

Mwenzako mi naogopaa! Mwenzako mi naogopa!

Wee vipi kwani una miaka kumi na mbili

Jamani mi naogopaa! aah! Jamani naogopaa!

Aaah! Acha zako! Naogopaa!

Unanitaka!

Hebu tulia *step* kulia

Nakupa muda uongee, nafasi uache kulia

Unanitega kwa *top* zisoshika mabega

Na bado una imani eti utaniteka

Vitendo kama sivioni na bado tuu nakumwaga

Kama laudhi za Pwani, njoo utafute mtoto wa kitanga

Nakupa nafasi ya kulonga unaogopa

Nikiondoka nyuma unachonga unaropoka

Kama maneno siyasikii kichwani hainiingii, hainijii

Kukaa uchi tu pekee hairidhii, haivutii

Usiseme na mwili sema na mimi

Vituko sivizimii maneno huniteka mimi

Kiitikio, Unanitega? Aaah! Mbona miguu ipo wazi?

Unanipenda? Aaah! Hebu uko! Mbona kifua kipo wazi?

Unanitega? Aaah! Mbona miguu ipo wazi?

Unanipenda? Aaah! Hebu uko! Mbona kifua kipo wazi?

Njoo useme

You actually think I want you? *Ofcoz*

Miguu wazi nimekubali, kifua wazi nimekubali sasa unataka niotee rangi ya

*G – String* una hatari.

Huu ni wimbo ambao ameutunga na kuuimba kwa kushirikiana na mwanamuziki mwenziwe Nurah wa kundi la *"Chamber Squad".* Maudhui ya wimbo nayo ni ya mapenzi, hili linadhihirishwa na mhusika wa wimbo ambaye ni mwanaume ambaye analalamika kuwa anapew vishawishi vya kimapenzi na mwanamke kwa vivazi anavyomvalia, tabia na vitendo anavyomfanyia. Kifani msanii ameupamba wimbo huu kwa kutumia lugha nyepesi ya Kiswahili isiyo na mafumbo mengi, misimu ya lugha, na lugha ya Kingereza kidogo. Mfano jina la wimbo "Unanitega" ni msimu wa lugha wenye maana ya unanishawishi,….

### 4.2.3 Vionjo Vya Kimapenzi Katika Nyimbo za Wasanii Teule

#### 4.2.3.1 Vionjo vya Kimapenzi Katika Nyimbo za Inspekta Haroun

##### 4.2.3.1(a) Vionjo vya Kimapenzi Katika Wimbo wa Asali wa Moyo

Asali wa moyo ni wimbo wenye vionjo kadhaa vya kimapenzi ambavyo vimetushawishi kuweka katika kundi la tungo za mapenzi. Miongoni mwa vionjo hivyo ni kama vile kitendo cha msanii kufananisha mpenzi wake ni kinywaji cha asali, huku akimpa nakshi zaidi mpenzi wake huyo kwa kumuita 'Asali wa moyo'. Kionjo kingine ni pale msanii anaposema kuwa anachanganywa kwa mengi sana na mpenzi wake huku akitaja sura, umbo na hata uhodari wa mapenzi kutoka kwa mpenzi wake huyo katika tungo hiyo;

"… Mwana wa Kahena, nimekufa kimahaba

Unanichanganya kwa mambo mengi sana

Kisura, kiumbo, mshobo mpaka uroda

Najua wanakutazama kwa jicho la husda mama

Mtoto kichungwa, kipotabo tena bomba…"

Mwisho, anasema kwa namna anavyompenda mpenzi wake hana shida na wala hajali jinsi jamii itakavyomuona. Bali yeye anaamini atafanya chochote atakachoambiwa na mpenziwe na hatojali jamii wakimuona kama ni zoba, mjinga ama poyoyo. Vilevile, msanii ametumia matumizi ya taswira zinazoonekana na hisi kama vile aliposema 'Kipotabo' maana yake mwembamba ni taswira inayoonekana na maneno kama 'mshobo','uroda' yote ni maneno yanayoonesha taswira hisi zenye maana ya kufanya mapenzi. Misingi ya idili za kiujumi za jamii zetu za kiafrika kuzungumzia masuala ya mahusiano ya mapenzi hadharani haziruhusiwi na kama zitazungumzia basi zitatumia lugha ya mafumbo kwa kiasi kikubwa ili watoto wasielewe kinachoimbwa.

**4.2.3.1(b) Vionjo vya Kimapenzi Katika Wimbo wa "Bint Kisura"**

Wimbo huu nao umesheheni vionjo vya kimapenzi kijidhihirisha kuwa ni utungo wa kimapenzi. Vionjo hivyo ni kwanza, msanii ameanza kutaja sifa za kimaumbile za binti huyo kuwa ana kifua (matiti) madogo ana *hips* kubwa na kajazia nyonga na akasema ana uzuri kama redio nzuri ya dabo deka(hapo zamani ilikuwa na thamani kipindi nyimbo hii inatoka). Kama alivyodhihirisha katika mistari ya wimbo huu;

"…Ana kifua konzi, sio mtindi chuchu kifuu

Akibonga analonga kama ana mafua kwa kizungu fluu

Kafungashia hips kajazia nyonga kaning'iniza cha bei mbaya
kilongalonga…"

Kionjo kingine kilichooneshwa katika wimbo huu ni maudhui yote ya wimbo huu ambao unaelezea namna wanaume vijana kwa wazee wanavyojitahidi kutoa ahadi za kumshawishi bint Kisura ili waweze kuwa na mahusiano ya kimapenzi na bint huyo.Hapa kuna matumizi ya taswira zinazoonekana kama vile 'kifua konzi', 'chuchu kifuu' maana yake matiti madogo, wakati neno 'mtindi' limetumika kuonesha matiti makubwa. Matumizi ya misimu kama Kubonga limetumika likiwa na maana ya kuongea, Kafungashia msimu wenye maana ya mwanamke mwenye umbo kubwa katikati ya mwili wake, Kilongalonga maana yake simu ya mkononi.

**4.2.3.1(c) Vionjo vya Kimapenzi Katika Wimbo wa "Mtoto wa Geti Kali"**

Wimbo huu nao una vionjo vya kimapenzi ambavyo vimetushawishi kuweka katika tungo za mapenzi. Kionjo kimojawapo ni pale msanii anapoanza kujinadi namna alivyompenda msichana ambaye wana tofauti kubwa ya kiuchumi. Licha ya tofauti hiyo ya mahali na maisha wanayoishi wote wawili, anamua kupiga moyo konde na kuweka tofauti hizo pembeni na kuelezea hisia zake. Kama mistari ya wimbo huo ilivyonukuliwa;

"…Sio siri kwa mtandao huu Inspekta nimeuawa kikatili
kwa kumpenda mtoto wa kikaladi, bambadi, uso softi usio
chunusi…, Kwao Obei, Osterbay, Masaki bint huyu
mtanashati…, Wakati msela Kabwela kajamba nani,
maisha uswahilini, Temeke Mikoroshini, sina hata Baiskeli…"

Vilevile, msanii ametuonesha vionjo vingine pale alipokuwa anaelezea wasifu wa nje wa msichana. Sifa hizo ndizo zinaibua vionjo vya kimapenzi katika jamii. Inspekta Haroun anasema;

> "…mdomo umekolea shedo lipstick, wa kunyonya
> denda bait *love romance,* ngozi nyororo, mororo
> murua, mwili utafikiri kamwagiwa asali, ana pua
> ndefu ndefu ya kikabachori, kila nikimchunguza
> sioni hata dosari, ama kweli kupenda ni sawa na
> donda ndugu…"

**4.2.3.1(d) Vionjo vya Kimapenzi Katika "Wimbo wa Asali wa Moyo (remix)"**

Wimbo huu nao una vionjo vya kimapenzi. Msanii anazungumzia namna mahusiano yake ya kimapenzi na mkewe Bi. Sada yalivyokumbwa na misukosuko. Walivumiliana na wala hawakuachana, licha ya kuwapo kwa kashfa za mwanaume huyo kuwa na uhusiano na wanawake wengine nje ya ndoa. Nukuu katika vipande vya mashairi ya wimbo huo inasema;

> "Penzi letu lilikumbwa na vikwazo sana
> Wewe ulivumili wala hatukuachana
> Walikwambia kila siku nabadili wasichana
> Uliwapuuza hukujali yao sana…"

#### 4.2.3.2 Vionjo vya Kimapenzi Katika Nyimbo za Mwanafalsafa

#### 4.2.3.2(a) Vionjo vya Kimapenzi Katika Wimbo wa "Alikufa kwa Ngoma"

Wimbo huu ni wa mapenzi ingawa si kwa wazi katika mashairi ya tungo hii. Ulitungwa na kuimbwa mahsusi kwa lengo la kuwahamasisha vijana kuacha tabia ya kujiingiza katika mahusiano ya kimapenzi bila ya kujua athari za kufanya hivyo. Yawezekana wakijihusisha katika mahusiano wanaweza kuingia katika janga la kupata magonjwa ya zinaa hata UKIMWI. Msanii anapomtaja mhusika wa kwenye utungo kwamba alikuwa na tabia ya kugawa kondomu kama Angaza. Katika wimbo huu vionjo vya kimapenzi vimedhihirishwa pale msanii alipokua anaelezea wasifu wa mhusika wa kwenye wimbo. Mathalani pale anaposema kuwa;

> "…Anayewaza kabla ya kusema. IBILISI wa njia za mwili
> Daima alimchezea mbali, tungi vicheche mineli
> Hakuonekana kujali, tazama maisha yake
> Hutaliona kosa lake, kama aliefunga kufuli
> katikati ya nyeti zake, mkali wa ushauri nasaha
> aliongea kuhusu mapenzi, huku akipinga zinaa…"

Vile vile, kuna matumizi ya misimu ambayo yamepamba mashairi ya wimbo huu kama vile 'vicheche' maana yake mwanamke Malaya, 'tungi' maana yake pombe, 'mineli, maana yake sigara, 'mshkaji' lenye maana ya rafiki, 'maskani, lenye maana ya sehemu ambayo vijana hukutana na kubadilishana mawazo.

#### 4.2.3.2(b) Vionjo vya Kimapenzi Katika Wimbo wa "Wanazimika"

Wimbo huu wakati mwingine hutambulika kwa jina la "Wanapendana". Katika wimbo huu, Mwanafalsafa ameonesha vionjo mbalimbali vya kimapenzi. Mathalani, ametaja baadhi ya viungo vya mwili/sehemu za mwili, hususani mwanamke kama vile vitovu, matiti na kutaja nguo ambazo hazimsitili mwanamke hata kidogo. Baadhi ya mistari yake ni;

> "…Napenda vitovu ila naogopa shanga labda bado
> mdogo au labda bado mshamba… wanapopiga
> mipasuo hawalengi jinsia yao nyie ndio kusudio…
> Wapo wanaovaa  vikuku ili kuleta picha ya ngono…"

Vilevile msanii amewatambulisha wanaume kama marijali kuwa wao ni kawaida yao kupenda, lakini wanawake wao hupenda zaidi katika mahusiano. Akaendelea kusema kuwa kuna wanawake ambao hupenda wanaume bila ya kujali wana hali gani za kiuchumi. Tofauti za kiuchumi sio suala la msingi katika mahusiano ya kimapenzi.

#### 4.2.3.2(a) Vionjo vya Kimapenzi Katika Wimbo wa "Hawajui"

Humu pia ametuonesha vionjo vya kimapenzi kwa kiasi fulani. Kwani, msanii amezungumzia mahusiano ya kimapenzi yanayoyumbishwa na tabia za mwanaume kutokuwa muaminifu katika ndoa. Mwanamuziki huyu ametudhihirishia vionjo vya kimapenzi katika mstari wa kwanza wa wimbo huu juu ya tabia ya mwanaume huyu asiye mwaminifu katika ndoa. Anasema;

"Suruali zinanifunguka vicheche vikikatisha, mshara
ukitoka sirudi mpaka unakwisha, nikirudi nane usiku
nalala na viatu, chicha chakari sikumbuki hata ndoa
yetu, nikiwa na wewe moyoni Napata aibu…"

#### 4.2.3.2(a) Vionjo vya Kimapenzi Katika Wimbo wa "Unaitega"

Wimbo huu una vionjo vya waziwazi vya kimapenzi waziwazi. Kwanza kabisa, jina la wimbo la 'Unanitega' ni la msimu wa lugha lenye maana ya kuwa unanishawishi/unanihamasisha. Mhusika wa kwenye wimbo analalamika kuwa anahamasishwa kuingia katika mahusiano na mtu kwa vitendo anavyofanyiwa bila ya kusema. Vilevile msanii anaonesha kuwa vitendo anavyofanyiwa na mwanamke wa kwenye wimbo huo kuwa ni vile vinavyohamasisha kuingia katika mahusiano naye ya kimapenzi na anampa fursa ya kuongea na aache vitendo bali aongee shida yake

"…Unaitega kwa top zisizoshika mabega na
bado una imani eti utaniteka vitendo kama
sivioni na bado nakumwaga…
…Kama maneno siyasikii kichwani hainiingii
kukaa uchi tu pekee, hairidhii, hainivutii usiseme
na mwili sema na mimi…"

## 4.3 Sababu Za Matumizi Ya Vionjo Vya Kimapenzi Katika Nyimbo Za Wasanii Teule

### 4.3.1 Kufikisha Ujumbe

Wasanii wengi wa kazi mbalimbali hufanya kazi zao kwa lengo kufikisha ujumbe kwa jamii wanyoiandikia kazi. Ujumbe hutolewa kama njia ya kuelezea hisia au tukio ambalo liliwahi kumpata mtunzi au mtu wa karibu na mtunzi/msanii wa kazi husika na hulifikisha kwa jamii kwa kutumia kazi hizi za sanaa. Ujumbe umekuwa ndio ngao ya wasanii kuwa ndio sababu ya msingi inayowasukuma wao kuandika nyimbo zenye vionjo vya mapenzi ili jamii ijifunze au iguswe na tungo ambazo zina vionjo hivyo. Swali la kujiuliza kama kweli ujumbe ndio sababu ya msukumo huo je, nyimbo zote ambazo zina vionjo vya kimapenzi hutoa ujumbe tarajali kwa jamii lengwa. Kuna baadhi ya nyimbo huwa na vionjo vya kimapenzi lakini hazina ujumbe isipokuwa hujaa lugha za matusi, Badala ya jamii kupata ujumbe na kujifunza kutoka kwenye tungo hizo hupata kinyume chake na hata kutotamani kusikiliza tungo hizo.

### 4.3.2 Kunasa/Kuvutia Soko la Biashara

Hii ni sababu nyingine inayowasukuma wasanii hawa wa muziki wa kizazi kipya kuwa ni mabadiliko ya soko la muziki huu, kuwa wasikilizaji wakubwa wa nyimbo za kizazi kipya ni vijana ambao hupenda tungo zenye vionjo vya mapenzi kwani ndizo zinazonunuliwa sana. Wasanii huwalazimu kutunga tungo hizo kwa kuzingatia soko la biashara ya muziki huu. Kutokana na mabadiliko ya kimaendeleo inawalazimu wanamuziki wa sasa kutunga nyimbo ambazo zinaendana na soko la muziki bila ya kujali zitakuwa na athari gani katika jamii, kama vile kimaadili ya jamii husika pamoja na kudumu kwa tungo hizo katika vituo vya habari kama redio na televisheni. Licha ya hayo, kutokana na wasanii kutunga kazi zao kwa kuzingatia

kigezo hicho pekee kumesababisha kuwapo kwa mrundikano wa kazi nyingi zilizochapwa (zisizo na ujuzi wala weredi wa kiutunzi), zina matusi ya wazi, kwani hazina lugha ya fiche kama ilivyokuwa katika kazi (nyimbo) za wasanii wa zamani, hususani, wa taarabu walivyokuwa wakielezea mambo mazito ya mapenzi tena kwa lugha nzito na fiche. Mfano mzuri wa wasanii wa zamani ambao walikuwa wanazingatia kipengele cha matumizi ya lugha kulingana na muktadha ni kama vile Juma Bhalo, marehemu Issa Matona, Ally Star na wengineo. Bado wasanii hawa walitumia weredi wao katika kufumba lugha katika kuelezea mambo mazito na uhakika wa kunasa soko la bidhaa zao ulikuwapo.

### 4.3.3 Athari ya Fasihi pendwa Katika Jamii

Aina ya tungo ambazo zina vionjo vya kimapenzi inaelezwa kuwa ni fasihi pendwa hususani kwa rika la vijana. Hii ni kama ilivyo kwenye riwaya pendwa inapendwa zaidi na vijana ambao ndio wanunuzi wakubwa wa kazi hizi. Matokeo ya utafiti yanaonesha kuwa mlipuko wa uandishi wa tungo zenye vionjo vya kimapenzi ni kipindi cha mpito ambacho uga huu wa sanaa unakipitia kama ilivyokuwa katika fasihi andishi kwenye mlipuko wa riwa pendwa miaka ya 1980 – 1990. Kwa kuwa sanaa hii ya muziki si maji mafu haina budi kupokea mabadiliko yote yanayotokea katika jamii ikiwemo hili kukithiri kwa nyimbo pendwa zenye vionjo vya kimapenzi.

### 4.3.4 Hulka za Binadamu

Matokeo ya utafiti yanaonesha kuwa binadamu hupenda kuandika au kufanya kazi katika vitu ambavyo wanapenda (hobbies). Hivyo basi, hii ni mojawapo ya sababu iliyowasukuma wasanii hawa wateule kutunga nyimbo zenye vionjo na mahadhi ya mapenzi. Zaidi ya hilo, kuna miktadha ya kiutamaduni nay a kijamii ambayo pia

hutoa msukumo kwa wasanii kutumia nyimbo zenye vionjo vya mapenzi. Jambo hili linatiliwa nguvu na msanii Mwanafalsafa anayejinasibu kuwa hupenda kuitumia kaida hii kwa kuwa yeye ni mzaliwa wa Tanga kunakosadikiwa kuwa ndiko iliko asili ya mapenzi. Kwake anaamini ni vigumu kujitenga na uandishi wa tungo zenye vionjo vya mapenzi kwani akijitenga na uandishi wa namna hii, vile vile, anaamini mja asili haachi asili.

### 4.4.5 Ithibati ya Uhuru wa Kisanaa

Matokeo ya utafiti yanaonsha kuwa utunzi wa nyimbo zenye vionjo vya mapenzi ni rahisi kuliko utunzi wa nyimbo nyingine kwani nyimbo hizi wakati mwingine hauzingatii urari wa vina na mizani wanachozingatia zaidi ni uimbikaji tuu wa nyimbo hizo. Utunzi wa tungo zenye vionjo vya mapenzi huwapa uhuru mkubwa katika kutunga kutokana na ukiukwaji wa kanuni za utunzi wa mashairi.

## 4.4 Athari Za Vionjo Vya Kimapenzi Katika Nyimbo Za Wasanii Teule

### 4.4.1 Tija Zipatikanazo

#### 4.4.1.1 Kuburudisha jamii

Kwa kiasi kikubwa wasanii wa muziki wa kizazi kipya huandika nyimbo zenye vionjo vya kimapenzi kwa lengo la kuburudisha jamii, kama sehemu ya maliwazo na kufurahia tungo hizo. Jamii huburudishwa na tungo za namna hii kutokana na kuwa huzungumzia mafanikio katika mahusiano, furaha ya mahusiano na vituko vya mahusiano.

#### 4.4.1.2 Kudumisha Mahusiano

Kupitia tungo ambazo zina vionjo vya kimapenzi husaidia katika kudumisha mahusiano ya wanajamii. Wanajamii hutumia nyimbo hizo kama kielelezo cha kujifunza kutoka kwa wale ambao msanii aliowaelezea katika tungo zao kuwa wamefanikiwa. Kwa mfano kupitia wimbo wa "Hawajui – Mwanafalsafa na Lady Jay Dee" ni wasikilizaji ambao huhamasishwa kuwa na uvumilivu katika mahusiano ya mapenzi kuwa ndio msingi wa kudumisha mahusiano hayo.

Wimbo huu wa "Hawajui Tulikotoka" – Mwanafalsafa na Lady Jay Dee ni wimbo ambao kwa kiasi gani unawahamasisha wapenzi kudumu katika mahusiano. Unafunza uvumilivu, kuelewana katika mahusiano na mifarakano ni kitu cha kawaida katika mahusiano muhimu kumaliza tofauti na kutafuta suluhu ya mfarakano huo.

#### 4.4.1.3Kukuza Msamiati wa Lugha

Nyimbo zenye vionjo vya kimapenzi mara nyingi huwa na misimu ya lugha mbalimbali ambayo hutumika kukuza msamiati wa lugha. Kwa mfano, misamiati kama vile asali wa moyo, la azizi, Kichuna lenye maana ya mpenzi, Buzi lenye maana ya mwanaume, demu lenye maana ya msichana, mlupo lenye maana ya mwanamke Malaya, Teja lenye maana ya mtu anayetumia madawa ya kulevya mfano Lady Jay Dee aliwahi kuimba wimbo uliojulikana kama teja wa mapenzi na misamiati mengineyo haya ni matokeo ya tungo zenya vionjo vya mapenzi. Misamiati hiyo ndiyo hukuza msamiati wa lugha ya Kiswahili.

#### 4.4.1.4 Kuelimisha Jamii

Nyimbo mbalimbali ambazo zina vionjo vya kimapenzi jamii hunufaika na elimu itolewayo kutoka kwenye tungo hizo. Miongoni mwa elimu itolewayo kupitia wimbo huu ni kama vile umuhimu wa kudumisha mahusiano na kuzuia kuvunjika kwa ndoa na kupunguza ongezeko la watoto wa mtaani. Miongoni mwa nyimbo ambazo zina vionjo vya kimapenzi ambazo hutoa elimu ni kama vile "Hawajui Tulikotoka" ulioimbwa kwa kushirikiana Mwanafalsafa na Lady Jay Dee ni wimbo unaohamasisha wanandoa kuwa wavumilivu katika ndoa kwa ajili ya kuilinda na kuitetea ndoa hiyo ili iweze kudumu. Nyimbo nyinginezo ni kama vile "Na Wewe Milele" ya Ray C, "Nashukuru Umerudi" ya Recho, "Nisamehe" ya Bob Haisa, "Tulizana" ya Barnaba, "Nakuhitaji" ya Christian Bella nyimbo hizo zote zinaelimisha watu wanaopendana kudumu katika mahusiano.

### 4.4.2 Madhara ya Nyimbo Zenye Vionjo vya Mapenzi

#### 4.4.2.1 Kujiingiza Katika Mahusiano ya Umri Mdogo

Kutokana na kusambaa na kusikilizwa kwa nyimbo ambazo zina vionjo vya mapenzi katika jamii, watoto na vijana wengi hujikuta wanaingia katika mahusiano wakiwa na umri mdogo. Watoto hutaka kuigiza yale ambayo yameimbwa katika nyimbo hizo na kuwa katika hatari ya magonjwa ya zinaa na hatari ya kupata UKIMWI. Mathalani, nyimbo ambazo zina vionjo vya mapenzi hutaja masuala hayo ya mapenzi na vihamasishi vya kufanya mapenzi kama vikuku, shanga, kondomu na vinginevyo kwa uwazi zaidi. Kitendo kinachowachochea vijana na watoto kutamani na hata kushawishika kujiingiza katika majusiano wakiwa na umri mdogo jambo ambalo ni hatari kwa afya zao.Mfano nyimbo kama 'Akadumba' ya Ney wa Mitego,

‘Wanazimika’ ya Mwanafalsafa, zote huwahamisha vijana katika suala la mapenzi kutokana na kutaja mambo ya kuwahamasisha ngono zembe vijana.

### 4.4.2.2 Mmomonyo wa Maadili Katika Jamii

Nyimbo ambazo zina vionjo vya mapenzi kwa kiasi kikubwa husababisha mmomonyoko wa maadili katika jamii. Vijana na watoto hupenda kuigiza yale ambayo yanaimbwa katika tungo hizo katika masuala ya mavazi kama vile vimini, milegezo mipasuo katika mavazi yao kupitia video za nyimbo hizo. Mavazi ya wanamuziki wa nyimbo hizi pamoja na yale ya wanenguaji wao hata wapamba jukwaa ni yale ambayo hayana maadili kwa kiasi kikubwa kitendo cha kuchochea mmomonyoko wa maadili katika jamii. Mathalani, mavazi ya waimbaji kama Shilole, Snura, Recho ambao wote hawa ni wasanii wanaoimba nyimbo za namna hii pindi wanapokuwa majukwaani hayana maadili na huchochea mmomonyoko wa maadili katika jamii.

### 4.4.2.3 Kudumaza kwa Ubunifu

Kwa kiasi kikubwa nyimbo ambazo zina vionjo vya mapenzi huwa hazina ubunifu katika utunzi wake. Nyimbo hizo zinakosa ubunifu kutokana na kuwa watu huimba nyimbo zao kwa lengo la kuburudisha tuu na hata huweza kukiuka kaida za uandishi. Ubunifu unakosekana katika nyimbo za namna hii kutokana na mrundikano wa tungo nyingi ambazo zina vionjo vya mapenzi. Kwa mfano, yawezekana nyimbo za wasanii wawili tofauti kuelezea kitu kimoja ambacho ni mapenzi wanachotofautisha ni majina ya wimbo na wahusika wa wimbo. Wasanii wa namna hii huimba kwa lengo la kupata hela za haraka bila ya kujali wimbo utadumu kwa muda gani katika jamii na kuacha athari zipi chanya kwa wanajamii.

#### 4.4.2.4 Ufinyu wa Mawanda

Kwa kiasi kikubwa nyimbo ambazo zina vionjo vya kimapenzi hukosa mawanda ya kuzungumzia tofauti na mapenzi tu. Nyimbo za namna hii kwa huwa ni chapwa (hazina upana wa fani na maudhui) kutokana na kuzungumzia dhamira moja tu ya mapenzi na kusahau dhamira nyinginezo za ujenzi wa jamii mpya na endelevu. Kutokana na ufinyu huo wa mawanda watu waliochoshwa ama kutendwa na mapenzi hawawezi kushawishika kusikiliza wimbo za namna hii kwani hazina dhamira mbadala na wala hawatapata ujumbe tofauti na wa mapenzi.

### 4.5 Muhtasari wa Sura ya Nne

Sura hii imejadili matokeo ya utafiti wetu. Nayo ni matumizi ya nyimbo zenye vionjo vya kimapenzi, sababu za matumizi ya nyimbo zenye vionjo vya mapenzi na mwisho ni athari za vionjo vya kimapenzi katika nyimbo za wasanii teule. Vile vile, katika utafiti huu imegundulika ya kuwa licha ya kuwa nyimbo ambazo zina vionjo vya kimapenzi zimekuwa zikipigwa vita kwa kiasi kikubwa katika jamii lakini zina tija sana katika ukuaji wa lugha ya Kiswahili. Hii ni kwa sababu kuna misamiati mingi ambayo imewahi kuibuliwa na wsanii wanaoimba tungo za namna hii ambazo mpaka sasa imekuwa ikitumika kukamilisha mawasiliano ya kila siku katika jamii. Pia utafiti huu umegundua kuna taarifa chache zinazohusu sanaa hii ya muziki wa kizazi kipya na wasanii na kuona ni jukumu la watafiti kuona sababu ya kuzamia katika uga huu wa sanaa ili kuweza kutafuta na kuhifadhi taarifa hizo kwa ajili ya vizazi vijavyo, Utafiti umegundua muziki wa kizazi kipya ni uga ambao hauna budi kuzamiwa kwa kufanyika tafiti mbalimbali kwani ni ajira endelevu kwa vijana ambao wana vipaji katika uga huu. Na sehemu kubwa ya pato la taifa endapoSerikali itamua kusimamia masuala ya udhibiti wa wizi za kazi za wasanii.

# SURA YA TANO

# MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

## 5.1 Utangulizi

Sura hii inadokeza muhtasari wa tasnifu hii na ina vipengele vinavyoelezea muhtasari wa tasnifu, hitimisho na mapendekezo kwa tafiti zijazo.

## 5.2 Muhtasari wa Tasnifu

Tasnifu hii ina jumla ya sura tano. Sura ya Kwanza imetambulisha usuli wa tatizo la utafiti, tamko la tatizo na utafiti, malengo, maswali ya utafiti na umuhimu wa utafiti. Sura ya Pili imejumuisha mapitio ya maandiko na nadharia zilizozotumika kama mwega wa utafiti. Sura ya Tatu imefafanua mbinu za utafiti pamoja na uwasilishaji na zana mbalimbali zilizotumika katika utafiti; ukusanyaji pamoja na uchambuzi wa data na uwasilishaji wa matokeo ya utafiti. Vipengele vilivyojuishwa ni mpango wa utafiti, eneo la utafiti taarifa za walengwa wa utafiti, vifaa vya kukusanyia data pamoja na udhibiti na uthabiti wa data. Sura ya Nne imejumuisha suala la uchanganuzi wa data; mjadala wa matokeo ya utafiti ambapo kila lengo mahsusi limebeba maudhui katika utafiti huu. Sura ya Tano imejumuisha muhtasari, hitimisho na mapendekezo. Pia kuna viambatisho mbalimbali kama vile picha na vielelezo vihusianavyo na utafiti huu.

## 5.3 Mapendekezo kwa Tafiti Zijazo

Kutokana na kuwa fani, hasa kipengele cha matumizi ya lugha katika kazi mbalimbali za fasihi hakijafanyiwa tafiti za kutosha kama ambavyo mawanda ya maudhui na historia ya muziki wa kizazi kipya yalivyoshughulikiwa. Hivyo watafiti

mbalimbali wanatakiwa waendeleze tafiti zao juu ya matumizi ya lugha na muziki wa kizazi kipya. Licha ya kuamini kuwa utafiti huu umeziba pengo lililokusudiwa kuzibwa lakini bado kuna maeneo mengi yanayopaswa kuzamiwa zaidi. Maeneo hayo ndiyo yanapendekezwa yafanyiwe utafiti ni kuhusu;

i. Athari za Muziki wa kizazi kipya katika kukuza na kuendeleza matumizi ya Kiswahili fasaha, na;
ii. Suala la ujumi wa Kiafrika katika nyimbo za muziki wa kizazi kipya.

## MAREJELEO


Almasi, A. (2012) “Mchango wa Muziki wa Hip hop Katika Kukuza na Kueneza Lugha ya Kiswahili nchini Tanzania”. Tasnifu ya Shahada ya Uzamili katika Fasihi ya Kiswahili, Chuo Kikuu Cha Dodoma. (Haijachapishwa).

Askew, K. (2002), *Perfoming the Nation*, Swahili Music and Cultural Politics in Tanzania, Chicago & London, Chicago University.

Baraza la Kiswahili Zaazibar (2010), *Kamusi ya Kiswahili Fasaha,* Oxford University Press, Nairobi.

Chachage, S. (2002), *Ndani ya Bongo*, Utandawazi na Migogoro ya Utamaduni, Idara ya Sosholojia, Chuo Kikuu cha Dar es salaam.

Chuachua, R. (2008) “Taswira katika Riwaya za Shaaban Robert” Ripoti ya Utafiti wa Kukamilisha Shahada ya Kwanza, Chuo Kikuu Cha Waislamu Morogoro, (Haijachapishwa).

Englert, B. (2003), “Bongo Flava Still Hidden Underground Rap From Morogoro”, Tanzania, Strichproben, Winer Zeitchrift fur Kritische Afikastudien. Vol 3, pp73-93.

Fenn, J. & Perullo A. (2000), A *Language Choice and Hip hop in Tanzania in Popular Music and Society*, University of Bowlin, Green city.

Jilala, H. (2008), “The Artistic Uses of Metaphors in Constructing Meaning and Messagea in New Generation Songs in Tanzania”. M.A. Dissertation, University of Dar es Salaam(Unpublished).

Kahigi, K. (1995), “Lugha katika Vitabu vya Watoto”, *Kioo cha Lugha*, Jarida la Kiswahili, Isimu na Fasihi, Idara ya Kiswahili, Chuo cha Dar es salaam, uk 145-166.

Kothari, C.R. (1990), *Research Methodology*, $2^{nd}$ edn, A Division of New Age International (P) Limited, New Delhi.

Kothari, C.R. (2009), *Research Methodology*, Method and Techniques ($2^{nd}$ Revised Edt.), New Age International Publishers Ltd, New Delhi.

Kraidy, M. (1990), *The Local, The Global and the Hybrid*: A Native Ethnography of Globalization. Critical Studies in Media Communication, vol 16 no 4, pp456-477.

Mandalu, M. P. (2008), "Factors affecting Unemployed Youth Effort toward Decent Work; The Case Study of Bongo Fleva in Dar es Salaam", Master Dissertation, University of Dar es Salaam(Unpublished).

Mangesho, P. (2003), *Global Cultural Trends*, The Case of Hip-hop Music in Dar es Salaam, M.A Dissertation, University of Dar es salaam(Unpublished).

Mbughuni, P. (1982), "The Image of Woman in Kiswahili Prose Fiction". *Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.* Juzuu 49(1), 15- 24.

Momanyi, C. (2001), "Nafasi ya Mwanamke Katika Ushairi wa Shaaban Robert". Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili, Juzuu 64, 53-64.

Msokile, M. (1993), *Misingi ya Uhakiki wa Fasihi*. EAEP ltd, Nairobi.

Mwamzandi, I.Y (2001), *Perfomance, Carnival and Deconstruction of Social Meaning* the Case of Taarabu among the Swahili in I.S Mdee and H.J Mwamsoko Pg 44-61.

Mzee, A.F. (2011), "Athari za Nyimbo za Taarabu ya Mipasho katika jamii ya Wanzanzibar". Tasnifu ya Shahada ya Uzamili katika Fasihi ya Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dodoma, Dodoma (Haijachapishwa).

Njogu, K. & R. M. Wafula (2007), *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi*, The JomoKenyatta Foundation, Sai Industries ltd, Nairobi.

Nyamahanga, A. (2012), "Matumizi ya Lugha katika Nyimbo za Kihehe Nchini Tanzania", Tasnifu ya Shahada ya Umahiri katika Fasihi, Chuo Kikuu Cha Dodoma, (Haijachapishwa).

Omari, S. (2006), "Mitindo na Matumizi ya Lugha Katika Muziki wa Kizazi Kipya", *Jarida la Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili*, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, vol 69, 73-93.

Omari, S. (2009), "Tanzanian Hip hop Poetry as Popular Literature", Unpublished Phd Thesis, University of Dar es salaam.

Perrullo, A. (2005), "Hooligans and Heroes", Youth Identity and Hip hop in Dar es salaam, Tanzania, Africa Today, vol 51, no.4, pp 74-101.

Perullo, A. (2003), "The Life That Live, Popular Urban Practice and Agency in Dar es salaam*" Tanzania,* Unpublished Phd, Dissertation, University of India.

Perullo, A. (2007) *Heres a Little Something Local An Early History of Hip hop in Dar es salaam*, Tanzania 1984-1997. Dar es Salaam: The History of Emeging East Africa Metropolis, ed by Andrew Burton, James Brennan & Yusuf Lawi. London: British Institute and James currey. pp 250 – 273.

Ponera, A. (2010), Ufutuhi katika Nathari za Shaaban Robert, Tasnifu ya Shahada ya Umahiri katika Fasihi, Chuo Kikuu Cha Dodoma.

Ponera, A. (2014), "Ufutuhi katika Nathari za Kiswahili: Ulinganisho wa Shaaban Robert na Euphrase Kezilahabi", Tasnifu ya Shahada ya Uzamivu katika Fasihi, Chuo Kikuu cha Dodoma (Haijachapishwa).

Ponera, A. (2015, "Misemo ya Kwenye Magari Kama Nyenzo ya Mawasiliano,"Muswada wa Makala uliotumwa kwa ajili ya Kuchapishwa katika *Journal of Himanities,* Chuo Kikuu cha Dodoma (Imechapishwa)

Remes, P.W. (1998), *Karibu Geto Langu/Welcome in my Ghetto* "Urban Youth Popular Culture and Language in 1990s Tanzania Phd dissertation, Howard University (University Microfilms No. 9832973)

Reuster-Jahn, (2007), *Lets Go Party!* Discourse and Self- Potrayal in Bongo Fleva Song Mikasi (Sex-Ngwair) Swahili Forum, vol 14, pp225-244.

Sanga, T.J. (2011), "Taswira ya Mwanamke Katika Mashairi ya Wasanii wa Kike wa Muziki wa Kizazi Kipya Tanzania". Tasnifu ya Shahada ya Uzamili Katika Fasihi ya Kiswahili, Chuo Kikuu Cha Dodoma, (Haijachapishwa).

Senkoro, F. (2003) "Rethinking Popular Arts & Culture in the 21st Century East Africa, Celebrating 30yrs CODESRIA.

Songoyi, E. M. (2005) "The Form and Content of Wigashe Dance Songs of the Sukuma", Tasnifu ya Shahada ya Uzamivu katika Fasihi, Chuo Kikuu Cha D'Salaam (Haijachapishwa).

Suriano, M. (2007), *"Mimi Msanii Kioo cha Jamii"* Urban Youth Culture in Tanzania as seen through Bongo fleva and Hip hop, *Swahili Forum* vol14. Pp 207-223.

TUKI (2004), *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*; Toleo la Pili, Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili, Dar es salaam.

Wamitila, K. W. (2002), "*Uhakiki wa Fasihi-Misingi na Vipengele Vyake",* Kenya Litho Ltd, Nairobi.

# VIAMBATISHO

## A. NYIMBO ZA MAPENZI KUTOKA KWA WASANII TEULE

## KIAMBATISHO 1

### A.1 Nyimbo za Mwanafalsafa

#### A.1.1 “Mi na Mabinti” – Mwanafalsafa

Kiitikio;

Wengine ndani ya jinsi, wengine ndani ya sketi, wengine ndani ya mini

Au magauni ya vitambaa vyepesi mradi istizahi wanipore uhuru wa nafsi

Weredi ajabu kwenye mambo chini ya paa

Kuna werevu ajabu kwenye mambo mengi *above*

Hawanipi shida sio balaa na zaidi nawapenda mabinti watundu

Mapozi ya kichokozi au sio pozi vurugu

Mitindo ya kiyahudi japo zikatazo kichwa

Na mikogo ya kifisadi sio makini napotosha

Unaona shanga za miguu unaita vikuku

Ingawa kwa wenyeufahamu ni upotofu

Watoto wa kibongo hakuna mchezo

Kuna Walatino Waafrika na Wasanta Domingo

Kuna mpasuo toka chini mpaka kando ya kiuno

Milango wazi yoyote aliye na mdomo

Sijapoteza macho kuangazia warembo

Nakosa uzalendo nionyeshwapo miguu

Napata uchizi wa mtima

Choma fedha na muda sioni balaa

Natumai sifunzi hasara ni hadithi sio biashara

Ukishindwa inshallah

**Kiitikio**

Kuna kifua kama cha Zay B, kiuno kama cha Ray C

Pozi kama za Jay Dee, sauti kama ya Fina

Au labda ya *Aunt* Ndina ipo njema

Matabasamu kama binti maumba wa kino

Msio nidhamu mtafanywa mpende ngono *hold on*

Kuna pozi za kimtoni kama Tausi Likokola

Unataka ni *full* bakora na mabinti wangali wanang'ara

Warefu warembo kama twiga mithili ya Happy Magese

Midomo kama Shose utapenda aonekane viwanjani yani ututese

Au binti maarufu utasema Ayna anatosha

Kama ntataka mwanya nafahamu wapi nitapata

Mwite Aminatha wa Keita binti wa Kigogo namtafuta

Mboni Ngita mwili utakaokufanya upende *love* kama

Mercy Garabawa na macho yanayovuta kama Miriam Ikoa

Unaweza utangazea ndoa wengine mziki kama Shanice

Au kama Konny Stevine na yote rangi Caroline

Na lugha tam kama ya Seven najua mnawaita sister duu

Bendera hawani sometime wavuta *weed mentally*

Japo wazuri mithili ya Kibibi miondoko kama Faudhia

Au ungependa  kithtethe mithili ya Radhia

Watoto wa shule wasiwafanye mpagawe

ilihali kuna wenye haiba kama Halima Bandawe

Mi kwa mabinti ni sahauliwe

Kiitikio;

Kunamabinti wapo kamili kila idara , familia bora

akili zisizo lala maumbo bora na sura

Kuwapata ni *full gospel* wao ni ajira

Na hawahitaji zaidi ya sera kuna mitego ya kanga

Mambo ya kitanga kama unajicho hii unapaswa kuwa umeiona

Michirizi ya utamu nyuma ya goti mi hoi na moyo hoi

Hii sio toi pigo nyingine kama *Sunset* ubishi haufai

Ona visa kwenye mitindo ya vichwa

Anwani pepe za mtandao na simu zinaweusha

Ukitaka upagawe njoo kiwanja

Jaribu kuwa mkweli uonapo vitovu wazi

Hakuna siri mahututi mimi kuna wadada, wamama

*Masister* duu wote wapenzi wananataka staki

So kamanda unaachia ngazi omba majina

Amina kawa maina Naima, Clara na Rayyah

Kuna Tayana, Anneth hata bongo kuna Alyah

Candis Cole Eunice au labda Mariah

Sikitu hataki jina na Asia anaitwa Eshiia

Pamba hazibani ni hatari ni makusudi tuone mistari ya kufuri mambo ya kivazi

Wachumba wote mko pina wote funga kazi hakuna

Msiache washkaji wafanye watumwa

Nyie ndio mama anaewaponda apate lana

Kiitikio;

Yaani shwari hamna shari

Mi na Mabint dam dam

Thamani ziko wazi mwenye macho aoneee

## B: MIONGOZO YA UDODOSAJI NA USAILI

**B: Mwongozo wa Usaili kwa Wataalamu kutoka BAKITA/TATAKI, Wanamuziki wa zamani, Watayarishaji wa muziki.**

Utafiti huu unahusu matumizi ya lugha katika muziki wa kizazi kipya, hususani, tungo za mapenzi zinavyoweza kuibua misimu mbalimbali ya lugha katika nyimbo teule za wasanii Inspekta Haroun na Mwanafalsafa. Vilevile, utafiti unalenga kuchunguza misimu hiyo inayoibuliwa kama inaendelea kutumika au imesanifiwa na kuwa lugha sanifu au imetelekezwa. Pia, utafiti unalenga kujua kama misimu hiyo inahusiana na maisha ya jamii za wasanii hawa.

1. Je, unafahamu tungo yoyote ya mapenzi ambayo imeimbwa na msanii Ispekta Haroun/ Mwanafalsafa. Kama ipo/zipo zitaje.
2. Je, unafahamu vionjo vyovyote vya kimapenzi katika tungo za wasanii wa muziki wa kizazi kipya (Inspekta na Mwanafalsafa) Kama ndio naomba vitaje angalau vitano.
3. Kila utanzu ya fasihi simulizi imekuwa ikitumia aina yake ya lugha. Je, muziki wa kizazi kipya unatumia lugha ya aina gani? Unadhani ni kwa sababu gani lugha ya namna hiyo inatumiwa?
4. Je, unadhani ni kweli matumizi ya lugha zisizo na kificho (lugha zilizo wazi) katika kuongelea masuala ya mapenzi zina athari katika jamii? Kama zipo, zibainishe angalau tano na kama hakuna toa sababu
5. Muziki wa kizazi kipya hususani ule ambao huimbwa kuzungumzia mapenzi hutumia lugha ambayo si ya kificho lugha ya wazi mno. Je unaweza kutaja sababu zinazowasukuma wasanii hawa kutumia lugha ya namna hiyo?

6. Je, unadhani jamii inaathirika vipi kutokana na kushamiri kwa tungo za muziki wa kizazi kipya ambazo zina vionjo vya kimapenzi hususani zile za wasanii (Mwanafalsafa na Inspekta Haroun )?
7. Unaweza kuwaelezeaje Inspekta Haroun na Mwanafalsafa kitabia? Je, unadhani kuna kushabihiana kokote kati ya maisha yao halisi ya wanamuziki hawa na fani na maudhui yanayojichomoza katika nyimbo zao?

***Asante kwa Ushirikiano Wako***

**B:2 Mwongozo wa usaili kwa Watu wazima wenye umri wa miaka arobaini na kuendelea**

1. Tunaomba utueleze kwa ufupi kuhusu jina na umri wako.
2. Je, unafahamu wimbo wowote wa msanii (Inspekta/Mwanafalsafa) ambao unazungumzia mapenzi? Naomba utaje/zitaje.
3. Je unaweza kubainisha vionjo vyovyote vya kimapenzi katika tungo hizo za mapenzi za wasanii teule (Inspekta/Mwanafalsafa)?
4. Unakumbuka simo/misimu yoyote ambayo imejitokeza katika wimbo/nyimbo uliyowahi kusikiliza ya/za wanamuziki hawa? Zitaje
5. Je unaweza kuelezea sbabu zinazowasukuma wasanii wa muziki wa izazi kipya kuandika wimbo/nyimbo ambazo zina vionjo vya kimapenzi katika jamii yao?
6. Katika kusikiliza muziki wa kizazi kipya unadhani muziki huu umetwaliwa na dhamira ipi/zipi kwa kiasi kikubwa.
7. Je, unadhani jamii ambayo wanasikiliza na kuufuatilia muziki wa kizazi kipya hususani ule wenye vionjo vya mapenzi wanapata athari zipi? Zitaje.
8. Je, unadhani muziki wa kizazi kipya hasa ule ambao una vionjo vya kimapenzi una faida yoyote katika jamii yako?

***Asante kwa Ushirikiano Wako***

**B:3 Mwongozo wa Mjadala wa vikundi kwa vijana wenye umri wa miaka (15-35)**

1. Mnaelewa nini kuhusu dhana ya matumizi ya lugha
2. Je, Mnazifahamu tungo za mapenzi kutoka muziki wa kizazi kipya hususani za wasanii(Inspekta/Mwanafalsafa)? Zitajeni.
3. Je, katika wimbo/nyimbo hizo kuna vionjo vyovyote vya kimapenzi? Kama vipo naomba mtutajie angalau vitano.
4. Je, mnadhani ni sababu zipi zinazowasukuma watunzi na wasanii wengi wa muziki wa izazi kipya hasa hawa wasanii teule kutunga nyimbo zenye vionjo vya kimapenzi katika jamii?
5. Je, nyimbo hizo zenye vionjo vya kimapenzi zinatumia lugha ya namna gani? Kuna misimu yoyote inayoibuliwa katika tungo hizo?
6. Je, kuna athari gani ambayo jamii huipata kutokana na kushamiri kwa tungo ambazo zina vionjo vya kimapenzi na dhana ya mapenzi?
7. Mna maoni gani kuhusu faida au hasara za kutumia nyimbo ambazo zina vionjo vya kimapenzi kwa mtu binafsi na kwa jamii?

***Asante kwa Ushirikiano Wako***